# UJENZI WA TASWIRA: DHIMA YA TASHIBIHI, SITIARI, TASHTITI NA MAELEZO YA MANDHARI KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA*

**NA**


**MARGARET NGINA MUASA**

**C50/80364/2015**


**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA YA MAHITAJI YA KUTUZWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**OKTOBA 2020**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

Sahihi------------------------------------------------ Tarehe---04/11/2020---------------------------------------

Margaret N. Muasa (C50/80364/2015)
(mtahiniwa)

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

Sahihi------------------------------------------------ Tarehe---5/11/20---------------------------------------

Prof. Kineene wa Mutiso

Sahihi------------------------------------------------ Tarehe---5/11/2020---------------------------------------

Prof. Tom Olali

## VIFUPISHO VYA MANENO

khj. - kama hapo juu/keshatajwa

mhar.- mhariri

wahar. - wahariri

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia wazazi wangu wapendwa; Thadeus Muasa na Mary Njoki. Walinitia moyo niendeleze masomo yangu. Aidha sitawaweka pembeni mume wangu Dickson Mutua na wanangu Maryanne, Mercy na Deborah. Walinivumilia na kunitia moyo wakati nilikuwa natia jitihada katika utafiti huu.

# SHUKRANI

Baada ya chombo kutia nanga, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia kufanikiwa kwa safari hii. Kwanza, namshukuru Maulana kwa kunipa siha njema. Vile vile alinipa stahamala ili nitimize azma yangu ya masomo.

Pili, ningependa kuwashukuru manahodha wasimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso na Prof. Tom Olali. Waliniongoza hatua baada ya nyingine. Walinikosoa kwa upendo usio na kikomo. Walinitia moyo hasa wakati nilizembea. Juhudi zao ni za kipekee. Aidha shukrani zaidi zimwendee Prof. Kineene wa Mutiso kwa kunipa tendi kadhaa ambapo nilichagua *Utendi wa Ngamia na Paa*.

Shukrani zingine nawapa wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi walionifunza. Bila shaka, iwapo hawangenielekeza vyema tasnifu hii haingefua dafu. Walinifaidi kwa msaada wao wa vitabu, makala, ushauri wao wa busara na kunitia moyo. Miongoni mwa hawa wahadhiri ni: Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Evans Mbuthia na Dkt. Jerono. Mungu awabariki nyote na awape hekima ya kuwaelekeza wanafunzi wengine.

Isitoshe, natoa shukrani za dhati kwa wanafunzi wenzangu tulioshauriana nao. Kwa mfano, Aloo Ronald, Mariga, Gloria na Mwaniki. Walikuwa tayari kunipa msaada wa hali na mali.

## IKISIRI

Katika utafiti huu, tumeshughulikia dhima ya tashibihi, sitiari, tashtiti na maelezo ya mandhari katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Utenzi huu ni miongoni mwa tenzi sita za Kiswahili za jadi zilizokusanywa, kuhaririwa na kutafsiriwa katika lugha ya Kiingereza na J. W. T Allen. Utenzi huu unahusu hadithi ya Ngamia na Paa na jinsi wanyama hawa wawili walitambua nafasi ya Mtume Muhammad katika kukomboa nafsi zao. Katika utafiti huu tumejikita katika kubainisha mchango wa tashibihi, sitiari, maelezo ya mandhari na tashtiti katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Pia tumechunguza iwapo taswira zinadhihirika wazi wazi kutokana na matumizi ya tashibihi, sitiari, tashtiti na maelezo ya mandhari. Isitoshe, tumechunguza iwapo mtunzi anapotumia mbinu hizi nne katika kazi ya kifasihi ataweza kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Tumetumia nadharia ya mtindo ili kupata mwelekeo wa utafiti wetu.

**FAHARASA**

UNGAMO........................................................................................ **Error! Bookmark not defined.**

VIFUPISHO VYA MANENO .................................................................................................... ii

TABARUKU ........................................................................................................................... iv

SHUKRANI.............................................................................................................................. v

IKISIRI .................................................................................................................................... vi

SURA YA KWANZA ................................................................................................................ 1

1.1 Usuli wa mada...................................................................................................................... 1

1.2 Tatizo la utafiti ..................................................................................................................... 2

1.3 Maswali ya utafiti................................................................................................................. 3

1.4 Malengo ya utafiti ................................................................................................................ 3

1.5 Sababu za kuchagua mada.................................................................................................... 4

1.6 Upeo na mipaka.................................................................................................................... 5

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo ............................................................................................... 5

1.8 Msingi wa nadharia .............................................................................................................. 7

1.9 Mbinu za utafiti ................................................................................................................... 16

1.9.1 Ukusanyaji data ............................................................................................................. 16

1.9.2 Uteuzi wa sampuli ......................................................................................................... 17

1.9.3 Uchanganuzi wa data..................................................................................................... 17

1.9.4 Uwasilishaji matokeo ya data ........................................................................................ 17

1.10 Mbeko za utafiti ................................................................................................................ 17

1.11 Hitimisho........................................................................................................................... 18

SURA YA PILI........................................................................................................................ 19

2.0 MATUMIZI YA MAELEZO YA MANDHARI KUUNDA TASWIRA KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA* ........................................................................................ 19

2.1 Utangulizi ........ 19
2.2 Dhana ya taswira ........ 19
2.3 Dhana ya mandhari ........ 22
2.4 Aina za taswira ........ 23
2.4.1 Taswira za kuonekana ........ 23
2.4.2 Taswira za maongezi na masikizi/kusikia ........ 29
2.4.3 Taswira ya kugusa ........ 32
2.4.4 Taswira ya kuonja ........ 33
2.5 Hitimisho ........ 34
SURA YA TATU ........ 35
3.0 MATUMIZI YA TASHIBIHI NA SITIARI KATIKA UJENZI WA TASWIRA ........ 35
KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA* ........ 35
3.1 Utangulizi ........ 35
3.2 Dhana ya tashibihi ........ 35
3.2.1 Aina za tashibihi ........ 37
3.2.2 Tashibihi wazi ........ 37
3.2.3 Tashibihi funge ........ 38
3.2.4 Tashibihi jozi ........ 38
3.2.5 Aina za tashibihi katika *Utendi wa Ngamia na Paa* ........ 39
3.3 Dhana ya sitiari ........ 41
3.3.1 Aina za sitiari katika *Utendi wa Ngamia na Paa* ........ 44
3.3.2 Sitiari sahili ........ 44
3.3.3 Sitiari tendi ........ 45
3.3.4 Sitiari dhana ........ 46
3.4 Hitimisho ........ 46

SURA YA NNE ........ 47
4.0 MATUMIZI YA TASHTITI KATIKA UJENZI WA TASWIRA KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA* ........ 47
4.1 Utangulizi ........ 47
4.2 Dhana ya tashtiti ........ 47
4.3 Sifa za tashtiti na matumizi yake katika *Utendi wa Ngamia na Paa* ........ 48
4.4 Hitimisho ........ 59
SURA YA TANO ........ 60
5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 60
5.1 Utangulizi ........ 60
5.2 Muhtasari wa sura ........ 60
5.3 Matokeo ya utafiti ........ 62
5.4 Muhtasari wa matokeo ........ 63
5.5 Mapendekezo ........ 63
MAREJELEO ........ 64

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa mada

Taswira ni mbinu ya lugha inayotumiwa kuwasilisha ujumbe maalum kwa njia ya kimafumbo. Taswira huwa ni lugha ambayo inachora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara akilini mwa hadhira. Aghalabu ujenzi wa taswira huhusisha matumizi ya mbinu tofauti za lugha kama vile tashibihi, sitiari na tashtiti. Pia ujenzi wa taswira huchochewa na matumizi ya maelezo yanayoibua hisia zinazozua taswira tofauti tofauti.

Taswira hutumika katika tanzu zote za fasihi ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. Hata hivyo, taswira hutumika katika ushairi na utenzi kwa kiasi kikubwa. Ushairi hutumia lugha ya mkato. Kwa hivyo, ni lazima taswira itumike ili ifidie upungufu wa maelezo katika tungo za kishairi. Senkoro (1988) anaeleza kwamba ushairi hutumia lugha ya mkato ambayo imepangwa kwa njia iletayo mizani au mapigo yanayolandana na maudhui aliyokusudia kutoa mshairi. Lugha hii ili iwe ya kishairi mara nyingi huwa ya kitaswira, nayo ni mbinu kuu itumiwayo na washairi kuufanya ushairi wao uwe hai zaidi. Washairi huitumia ili kuzinasa hisia za hadhira kwa kuwapangia maneno yanayoweza kuumba picha kamili katika akili zao.

Aidha, Njogu na Chimerah (1999) dhana ya ushairi wanaifafanua kwa kusema kuwa ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilikaji. Maneno ya mashairi huteuliwa kimakusudi (ili yalete taswira maalum akilini mwa msomaji au msikilizaji).

Ni dhahiri kuwa matumizi ya taswira ni muhimu katika ushairi hususan tenzi. Tenzi au tendi huhusisha matumizi ya beti nyingi. Utenzi ni utungo wa kishairi wenye kusimulia tukio fulani maalum kwa kutumia maelezo. Aidha, utenzi ni hadithi ndefu ambayo imeandikwa kwa njia ya ushairi. Hivyo basi ni lazima mtunzi atafute njia ya kunata makini ya msomaji ili aweze kumudu kusoma beti zote. Taswira huwa nyezo muhimu ya kutoa maelezo haya yanayopatikana katika utenzi.

Aghalabu matumizi ya taswira hufaa kwa sababu hadhira inaweza kupata uhalisia au picha ya ujumbe unaowasilishwa na mtunzi. Mathalani, katika *Utenzi wa Ngamia na Paa*, ngamia na paa wanaweza kuzungumza. Jambo hili litazua taharuki na litachochea msomaji awe na hamu ya

kutaka kujua yale ngamia na paa watakayoyasema. Taswira humwezesha mshairi au mtunzi wa utenzi kuwasilisha dhana, hali au mawazo yake kwa njia ya: mkato (sifa kuu ya ushairi/utenzi), rahisi na yenye mvuto zaidi. Hali kadhalika, mtunzi huweza kuwasilisha mawazo yake kwa njia yenye uhalisia. Yaani mpokezi au msomaji wa ile kazi anaweza kuilinganisha na mandhari halisi ya ulimwengu wa kihalisia.

Katika utafiti huu, tumeangazia taswira katika *Utendi wa Ngamia na paa*. Utendi huu una takribani beti 384. Ni miongoni mwa tenzi sita za Kiswahili za jadi zilizokusanywa, kuhaririwa na kutafisiri katika lugha ya kiingereza na J.W.T. Allen. Tenzi hizo zingine ni *Utenzi wa Mwanakupona, Utenzi wa Masahibu, Utenzi wa Mikidadi na Mayasa, Utenzi wa Ayubu* na *Utenzi wa Kiyama.*

Utenzi huu unahusu hadithi ya Ngamia na Paa na jinsi wanyama hawa wawili walitambua nafasi ya Mtume Muhammad katika kukomboa nafsi zao. Kwa mfano, Ngamia anakuja kumwomba ili amtetee. Ngamia alikuwa katika hatari ya kuangamizwa na Bwana wake, Abu Masud, ambaye alikuwa kafiri. Ngamia aliteswa licha ya kufanya kazi ya kumtumikia Bwana huyu kwa kila hali.

Wahakiki wengi wameshughulikia tamathali za lugha katika tenzi kadhaa na kazi zingine za fasihi hasa tashbihi na sitiari. Hata hivyo, taswira haijashughulikiwa kwa kina. Azima yetu imejikita katika kuchanganua dhana hii ya taswira na kubainisha mbinu mbalimbali zilizotumiwa kuijenga katika *Utendi wa Ngamia na Paa*.

### 1.2 Tatizo la utafiti

Uwasilishaji wa mawazo ya mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi huweza kufanikishwa kupitia matumizi ya mbinu mbali mbali za kifasihi na za lugha. Taswira ni mojawapo wa kiungo muhimu cha kuwasilisha ujumbe wa fasihi. Taswira huweza kujitokeza pekee bila ya kuegemea katika mbinu zingine za lugha; ikahusisha maelezo yanayohusu vitu vinavyopatikana katika mazingira ya hadhira. Hata hivyo, taswira aghalabu hujengwa kwa tamahali za usemi kama vile tashibihi na sitiari. Mathalan, Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa ili kujenga taswira mtunzi mara nyingi hutumia tamathali mbili za usemi; jazanda na tashibihi.

Pia kuna mjadala kuhusu taswira zinazoundwa na maelezo pekee na zinazoundwa na tamathali zingine za lugha. Baadhi ya wahakiki wa kazi za kifasihi wanasema kuwa taswira zinazoundwa na tamathali pekee hazipaswi kutumiwa kama kigezo cha kuangazia taswira kwani hata zile

zinazohusu maelezo ni muhimu pia. Kwa mfano, Ngunjiri (2012) anasema kwamba sio lazima tamathali za semi zisheheni taswira ya kimaandishi bali ni uteuzi wa msamiati na ubunifu wa lugha utakaoibua hisia za msomaji au msikizi. Aidha anasisitisa kwamba matumizi ya tamathali za usemi ni mojawapo wa visaidizi vya kuunda taswira na wala sio kaida ya kufuatwa kwa lazima ili kigezo cha taswira kiafikiane.

Maoni kama haya yametupa mshawasha wa kuzua maswali yafuatayo: Je, mbinu hizi (tashibihi, sitiari, maelezo ya mandhari na tashtiti) zina mchango wowote katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa?* Je, taswira inadhihirika wazi wazi kutokana na matumizi ya tashibihi, sitiari, tashtiti na maelezo ya mandhari? Je, wakati mtunzi anapotumia mbinu hizi nne katika kazi ya kifasihi ataweza kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe?

Hivyo basi, katika utafiti wetu tumechunguza namna tashibihi, sitiari, tashititi na maelezo ya mandhari yanachangia katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Tofauti na wahakiki watangulizi wetu kama vile, Momanyi (1991), Tambasi (2011), Karanja (2014) na Nzilu (2018).Watafiti hawa walishughulikia taswira kama kipengele kinachojitegemea bila kukihusisha na tamathali zingine. Pia walishughulikia kazi tofauti za kifasihi tofauti na utafiti wetu wa *Utendi wa Ngamia na Paa*.

### 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

1. Je, taswira alizotumia mtunzi zinafaa na zinaweza kunasibishwa na ulimwengu halisi uliochota ufafanisho kutoka kwa fasihi simulizi?
2. Je, aina mbali mbali za taswira zimejitokeza kwa uwazi katika utenzi huu?
3. Je, mtunzi amefanikiwa kutumia tamathali na mbinu zingine za lugha (kama vile, tashbihi sitiari, tashititi na maelezo ya mandhari) katika kujenga taswira mbali mbali?

### 1.4 Malengo ya utafiti

Kazi hii imelenga;

1. Kubainisha jinsi tashibihi, sitiari, tashititi na maelezo yametumiwa katika kuumba taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*.
2. Kufafanua aina za taswira ambazo zimeumbwa katika *Utendi wa Ngamia na Paa*.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tumeshughulikia mada hii kwa sababu kadha. Kwanza, uchaguzi wa mada hii umechochewa na lugha ya utenzi huu ambayo ni chakavu. Uchunguzi wa ujenzi wa taswira umetuwezesha kuiweka bayana. Jambo hili litasaidia wasomi na watafiti wengi kuelewa ujumbe wa utenzi huu kwa urahisi. Kwa mfano, tenzi hasa za zamani zilitumia msamiati wa lugha ya Kiarabu, maelezo yanayofungamana na dini ya Kiislamu na lahaja mbali mbali za Kiswahili. *Utenzi wa Ngamia na Paa* umesheheni misamiati hii. Kwa mfano, katika utenzi huu neno ngamia limekuwa likitumiwa katika baadhi ya beti. Aidha neno la kiarabu jamal linalomrejelea ngamia yule yule likitumika katika beti zingine.

Licha ya utenzi huu kuhaririwa zamani na Allen (1971) wahakiki wengi hawajaushughulikia. Katika uchunguzi wetu tumegundua kuwa wahakiki wengi wameshughulikia tenzi zijulikanazo au maarufu. Kwa mfano, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Mwanakupona.* Hata hivyo kuna tenzi nyinyi tofauti za fasihi ya Kiswahili ambazo hazijachunguzwa. Kwa hivyo tumedhamiria kuwachochea wahakiki wengine waweze kuziba pengo hili kwa kutafiti kuhusu tenzi hizi au kuuhakiki *Utenzi wa Ngamia na Paa* kwa kuangazia vipengele vingine vya kifasihi.

Isitoshe, kama jinsi tumekwisha taja katika usuli wa mada, taswira ni fumbo. Taswira hulenga kuifikirisha hadhira ili iweze kupata maswala yanayoathiri jamii. Kwa hivyo, uhakiki huu umenuia kumsaidia msomaji kupata mshawasha wa kuyachunguza yale mafumbo yanayojengwa na taswira mbali mbali katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Na jinsi yametumika kuwasilisha maswala muhimu katika jamii.

Ujenzi wa taswira haujachunguzwa kama mada mahsusi ya utafiti katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Katika utafiti uliofanywa na Allen (khj.) alijikita katika kukusanya na kutafsiri tenzi sita za kale. Tenzi hizi tumezitaja katika usuli wa mada. Aidha alizitolea maelezo mafupi. Kwa mfano, anasema kwamba *Utendi wa Ngamia na Paa* ni mfano wa hurafa. Pia anatoa mifano mingine ya kazi zinazofanana na hii kama vile *Kozi na Ndiwa* na *Shufaka*. Kwa hivyo, uchunguzi wa ujenzi

wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa* umerahisisha ufahamu wa ujumbe wa utenzi huu zaidi.

### 1.6 Upeo na mipaka

Tumeshughulikia jinsi tashibihi, stiari, tashititi na maelezo ya mandhari yanavyochangia ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Hatukuangazia tenzi zile zingine zilizotafsiriwa na Allen (1971) kama tulivyokwisha zitaja. Vile vile kwa kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya fani na dhamira, wakati mwingine imetulazimu kutaja dhamira zinazosawiriwa katika taswira hizi lakini kwa kifupi.

Ili kuhakiki kazi hii kitaaluma tumejikita katika nadharia ya mtindo. Nadharia hii imetufaa kwa sababu kimsingi mtindo huwa na maana ya kurejelea jinsi lugha inavyotumika katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Vile vile mtindo ndio husisimua au huibua msukumo wa kuifanya hadhira ipende kusoma au kusikiliza kazi ya fasihi.

### 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo

Wahakiki wengi wa kazi ya fasihi wameweza kuangazia taswira katika kazi mbali mbali za fasihi zikiwemo kazi za kinathari na kishairi. Aidha, mengi yameandikwa kuhusu vipengele mbali mbali vya tenzi mbali mbali. Ila machache yameangaziwa kuhusu uchanganuzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.*

Senkoro (1988) amefafanua maswala mbali mbali katika ushairi. Kwa mfano, ameeleza kipengele cha taswira katika ushairi. Amechambua aina za taswira katika mashairi tofauti tofauti kama vile mashairi ya Abdilatif Abdala kwa muhtasari. Pia ametoa maelezo kuhusu tenzi kadha kama vile *Utenzi wa Mwanakupona* na *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar*. Maelezo yake yametufaa katika kupanua uelewa wa mada yetu; hasa katika kufafanua aina mbali mbali za taswira.

Momanyi (1991) alichunguza uhusiano wa kuanguka kwa mji wa Pate na matumizi ya taswira katika *Utenzi wa Al-Inkishafi*. Katika utafiti wake alifafanua aina za taswira kwa kuangazia mazingira halisi yaliyoandikwa katika utenzi huu wa *Al-Inkishafi*. Utafiti huu ulitufaa kwa sababu tulijikita katika kutalii maelezo yaliyozua taswira na kuangazia jinsi mbinu za sitiari na

tashibihi zilivyozua taswira mbalimbali katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Pia unafanana na wetu kwa sababu ulichunguza tenzi.

Osiemo (1997) Katika utafiti wake, alihakiki fani kwa jumla alizotumia Hassan Mwalimu Mbega katika utunzi wake. Kazi yake ni ya manufaa kwetu. Maadamu imetuwezesha kupata maana mbali mbali za tamathali za semi pamoja na matumizi. Ijapokuwa alihakiki mashairi ya arudhi. Pia alitumia nadharia ya urasimu ilihali utafiti wetu umehusisha matumizi ya nadharia ya umtindo.

Nzuki (2003) uhakiki wake uliangazia jinsi maudhui kama vile siasa, mazingira, utamaduni na dhuluma ya kimapenzi yamejengwa kupitia tamathali mbali mbali za lugha. Utafiti wake ulijikita katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Kazi yake imetufaa kwa sababu imetusaidia kupanua mada yetu kuhusu ujenzi wa taswira. Hata hivyo utafiti wake na wetu umetofautiana kwa njia kadha. Kwanza, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya umtindo. Wa Nzuki (khj) umeongozwa na nadharia ya umuundo na kisosholojia. Pia utafiti huu umechunguza utenzi ilihali wake umehakiki ushairi wa kisasa.

Wamitila (2003) ametoa maelezo kuhusu istilahi tofauti tofauti za fasihi. Kwa mfano, amesema kwamba taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za ki-ishara. Taswira huweza kuundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashibihi na sitiari. Amesisitiza kwamba ingawa kimsingi taswira nyingi ni taswira za uoni; taswira za aina nyingine hujitokeza. Taswira hizi ameziorodhesha kama vile: taswira kuu, taswira ya kimsingi, taswira za harufu, taswira za mnuso, taswira za kimaelezo, taswira za kiishara, taswira za joto, taswira za mguso, taswira za mwendo, taswira za mwonjo, taswira za usikivu na taswira za wengine.

Japo maelezo ya Wamitila (khj.) yanahusu fasihi kwa jumla maelezo yake yametufaa katika kupata msingi wa utafiti wetu. Uainisho wa mtaalamu huyu umetufaa pakubwa kwa kuwa umetusaidia katika kufafanua baadhi ya aina za taswira. Hususan taswira zinazojitokeza katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Pia umetuchochea kuangazia jinsi mbinu za tashbihi na sitiari zimetumiwa katika kujenga taswira.

Nyanchama (2004) alichanganua mafumbo yanayopatikana katika mashairi mbali mbali katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Alizingatia taswira na ishara zilizotumika. Ingawa alijikita katika mashairi ya arudhi kazi yake imetusaidia katika kupanua mawanda ya utafiti wetu kuhusu ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.*

Lugwiri (2011) alifafanua dhana tatu za tamathali za semi (sitiari, taashira, na tashibihi) na mchango wa dhana hizi katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Utafiti wake umetufaidi kwa kuwa tumepata mtazamo tofauti wa tamathali hizi za semi. Isitoshe, utafiti wa Lugwiri (khj.) umefaa utafiti wetu kwa sababu ametumia nadharia ya umtindo ambayo vile vile tumeitumia katika utafiti wetu. Kwa hivyo amechochea uchunguzi wetu kuhusiana na nadharia hii.

Ngunjiri (2012) amechunguza jinsi taswira imetumika kufanikisha maudhui katika *Utendi wa Siraji*. Ametumia nadharia ya maadili katika kazi yake. Hata hivyo utafiti wake umetufaa kwa sababu umeangazia mbinu ya taswira ambayo tumeichunguza.

Mwakio (2016) ametufaa kwa sababu ameeleza kuhusu aina mbali mbali za tashibihi, sitiari, na taashira katika *Damu Nyeusi na hadithi nyingine*. Pia amehakiki kazi yake kwa kutumia nadharia ya umtindo ambayo vile vile tumeitumia kuhakiki *Utendi wa Ngamia na Paa.* Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa vile alihakiki hadithi fupi ilihali sisi tumehakiki *Utendi wa Ngamia na Paa.*

*Pungwa*, *Kivuli*, na *Mashetani Wamerudi* ambazo ni tamthilia tatu za Said Ahmed Mohamed zimehakikiwa na Nzilu (2018). Ametathimini matumizi ya taswira katika kueleza dhamira zinazojitokeza katika tamthilia hizi tatu. Kazi yake imekuwa muhimu kwetu kwa sababu imetuelekeza katika kutathimini aina mbalimbali za taswira. Aidha sawia na ilivyokuwa katika utafiti huu ametumia nadharia ya umtindo. Utafiti huu wa Nzilu umetofauti na wetu kwa vile umejikita katika uchanganuzi wa tamthilia ilihali wetu umejikita katika uchanganuzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.*

### 1.8 Msingi wa nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya mtindo. Nadharia hii imetufaa kwa kuwa waasisi wake na wataalamu ambao waliifafanua walijikita katika kuangazia jinsi lugha hutumiwa katika kazi ya fasihi. Kazi ya fasihi haiwezi kuwasilishwa katika jamii bila lugha. Mafanikio ya kuwasilisha ujumbe wa fasihi huegemea katika matumizi ya lugha au mbinu za lugha zilizotumiwa.

Lugha ni kiungo muhimu kinachomwezesha mtunzi wa kazi ya fasihi kuwasilisha mawazo yake katika hadhira. Hatuwezi kutenganisha ujumbe wa kazi ya fasihi kutoka kwa lugha. Wamitila (2003) akieleza maana ya fasihi anasema kwamba ni kazi za kisanaa au zilizotumia lugha kwa usanii na zinazowasilisha suala fulani pamoja kwa njia inayoathiri, kugusa na kuacha athari fulani na kuonyesha ubunilizi na ubunifu fulani na zinazomhusu binadamu. Hivyo basi lugha ndio msingi wa fasihi.

Kwa maoni yetu, mtindo ni jinsi msemaji au mwandishi huwasilisha kazi yake ili iweze kuvutia hadhira. Hali kadhalika, mtindo huchochea athari fulani kuachwa katika akili ya hadhira ili iweze kukumbuka ujumbe uliokuwa ukiwasilishwa. Nadharia hii imefaa katika utafiti wetu kwa kuwa tumejikita katika kuangazia ujenzi wa taswira kwa kutumia baadhi ya mbinu za lugha kama vile tashbihi, sitiari na tashtiti. Aidha tumeangazia jinsi ujenzi wa taswira umechochewa na matumizi ya lugha katika mandhari tofauti.

Aidha, mtindo ni ule upekee wa kuyaeleza mambo ya kawaida kwa njia ya kisanii. Hivyo basi kwa mjibu wa nadharia hii ya mtindo, msanii anapaswa kuteua mbinu za lugha zitakazomwezesha kujieleza kikamilifu. Uteuzi wa mbinu hizi za lugha hauwi bila masharti na kaida za kufuata. Kuna sababu ambazo humfanya msanii ateue mbinu moja na kuacha nyingine. Kwa mfano, ushairi/utenzi hujikita zaidi katika taswira kwa sababu ushairi hutumia lugha ya mkato. Pia katika utenzi, mtunzi hulazimika kutumia taswira kwa sababu utenzi ni hadithi ndefu iliyoandikwa kwa njia ya kishairi.

Nadharia ya umtindo ina mihimili kadhaa ila utafiti wetu umeongozwa na nguzo zifuatazo. Kwanza, lugha ndicho chombo tekelezi na huwa muhimu katika kueleza ujumbe uliokusudiwa. Nguzo hii inafaa katika utafiti huu kwa sababu imetuwezesha kubaini vipengele vya lugha vilivyotumiwa. Pili, upo usawa kati ya ujumbe na lugha ambao huchangia ufanisi wa kazi ya fasihi. Mwingiliano huu hauwezi kutenganishwa. Nguzo hii vile vile ni muhimu kwa sababu hutumika katika uzuaji na ubunifu wa kazi za fasihi. Mhimili huu ni wa manufaa katika utafiti wetu kwa sababu tumengazia taswira na jinsi mbinu zingine ambazo zimetumiwa kuijenga zimechangia uwasilishaji wa ujumbe katika *Utendi wa Ngamia na Paa.*

Nadharia ya mtindo iliwekewa msingi na Geoffrey Leech (1969). Hata hivyo ilikuwa imeanza kuelezwa katika miaka ya hapo awali na wataalamu kama vile Buffon. Wamitila (2003) akimrejelea Buffon anasema kwamba Buffon alieleza kuwa mtindo ni mtu mwenyewe.

Leech (1969) alieleza kwamba mtindo ni uchunguzi wa jinsi lugha imetumika katika fasihi. Isitoshe, lugha ni chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Alisisitiza kuwa fasihi haiwezi kuchunguzwa kwa undani bila kuzingatia uchunguzi wa matumizi ya lugha. Aidha anasema kwamba kazi ya fasihi hukusudia kuwakilisha hisia au tajiriba fulani kwa wasomaji. Tajiriba hizi hupitishwa kwa kutumia lugha. Anaendelea kusema kuwa tajiriba ya mwandishi atakayoiwasilisha kwa wasomaji ni kile anachochota kutoka kwa ghala la wanajamii wake. Wasanii wanapaswa kutumia lugha kwa namna isiyo ya kawaida ili waweze kuteka fikra za wasomaji wa kazi ya fasihi.

Leech (khj.) anasisitiza kwamba ili lugha ya kitamathali (kifasihi) ielezwe vyema mbinu za kiisimu zapaswa kuzingatiwa. Hali hii ya kuhusisha mbinu za kiisimu katika kuchanganua lugha ya kifasihi husababishwa na ugumu unaojitokeza wakati wa kufafanua msamiati wa kimsingi wa uhakiki wa fasihi kama vile sitiari, taswira, kinaya, usambamba na jazanda.

Miaka ya baadaye Leech (2007) aliungana na Short ambapo walieleza nadharia hii kwa uwazi zaidi. Wanasisitiza kwamba neno mtindo hurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Leech na Short (2007) wanapoeleza kuhusu njia ya kuhakiki kazi za kinathari za fasihi kwa kutumia mtindo wanasema kwamba kuna vigezo vinne ambavyo vinaweza kutumiwa ili kutoa mwelekeo wa kufuatwa. Kigezo cha kwanza kinahusu leksika (neno). Katika kigezo hiki aina mbali mbali za maneno huchunguzwa kwa mfano nomino, viwakilishi, vivumishi, vielezi n.k. Kwa maoni yetu, kila neno katika utungo huwa na maana. Msanii huteua maneno yatakayomwezesha kuyaeleza kisanaa mambo ya kawaida.

Kigezo cha pili kwa mujibu wa Leech na Short (khj.) kinahusu sarufi. Katika kitengo hiki aina za sentensi uangaziwa.Yaani uchangamano wa sentensi, hasa aina za virai. Kigezo cha tatu kinahusu tamathali za semi. Katika kigezo hiki tamathali za usemi kama vile jazanda, chuku, takriri, taswira, tashibihi na kadhalika huchanganuliwa. Kigezo cha mwisho kinahusu mwingiliano wa muktadha.

Kigezo cha tatu ndicho kimetufaa zaidi kwa sababu kinahusiana na utafiti wetu yaani ujenzi wa taswira. Tumejikita katika vipengele vingine vya matumizi ya lugha kama vile tashibihi, sitiari na tashtiti. Kwa mfano Leech na Short (khj.) wanasema kwamba mhakiki anapaswa kuangaza iwapo pana ukiukaji wa sheria za kiisimu ambao wanaurejelea kama *tropes*. Ukiukaji huu hutumika katika kueleza baadhi ya tamathali za usemi hasa zinazopatikana katika ushairi kama vile jazanda, kinaya n.k. Wanaendelea kusema kuwa jazanda zinahusiana na tashibihi hivyo basi ni vyema kuzihusisha kakika kitengo hiki.

Pia mwaka huo huo wa 1969 Crystal na Davy walitoa mchango wao mkubwa kuhusiana na nadharia hii. Kwa muhtasari wanasema kwamba nadharia ya kimtindo inapaswa kutusaidia kutambua jinsi lugha moja ina matumizi tofauti katika jamii. Vile vile wanaendelea kueleza kwamba mtindo unaweza kuelezwa kwa kutumia vigezo vinne: upekee wa mtu wa kutumia lugha. Pili mtindo hurejelea baadhi ya tabia au tabia zote zinazohusu matumizi ya lugha zinazotumiwa na kikundi cha watu. Tatu, mtindo huweza kuwa na maana ya kusema kinachopaswa kusemwa na kwa njia mwafaka zaidi. Mwisho mtindo una maana ya matumizi ya lugha ya kitamathali inayohusishwa na fasihi. Kijelezi cha tatu na nne kimetufaa katika kuchambua mada yetu.

Watafiti mbali mbali wameweza kutoa maelezo zaidi kuhusu nadharia hii ijapokuwa maelezo yao yanakaribiana na ya wasisisi wa nadharia hii kama tulivyokwisha eleza. Wamitila (2003) anafafanua zaidi dhana hii ya mtindo na kusema kuwa hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Tunaweza kueleza mtindo kama jinsi mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake, uakifishaji wake na kadhalika. Kila mwandishi ana mtindo wake pekee.

Wamitila (2008) anasema kuwa kauli ya Buffon “Mtindo ni mtu mwenyewe” ina ukweli wake kwa kiasi kikubwa. Ila inafifiza mchango wa muktadha katika kuunda mtindo. Hivyo basi, mtindo unaweza kuhusishwa na kipindi maalum cha kihistoria au watunzi wanaopatikana katika kipindi hicho fulani licha ya wenyewe kuwa na tofauti ndogo ndogo za kibinafsi. Katika utafiti

huu wetu hatujajikita katika maana hii ya mtindo inayozunguka mwandishi wa utenzi. Tumejikita katika muktadha (utenzi wenyewe) ambapo tumetathimini jinsi lugha ilivyotumika katika kuwasilisha ujumbe wake.

Nyutu (2016) akiwanukuu wana-umtindo Crystal na Davy anasema kwamba tunaweza kuhusisha mtindo na mazoea ya matumizi ya lugha ya mtu binafsi au jamii-lugha na hii ndiyo maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu mtindo wa uandishi wa mtu fulani, mtindo wa kuzungumza, wa kutoa hotuba hadharani na kadhalika. Maelezo haya yanakaribiana na yaliyotangulia yaliyotelewa na Wamitila akimnukuu Buffon.

Wamitila (2008) amefafanua zaidi kuhusu mtindo kwa kusema kwamba, nadharia ya umtindo ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa matini za fasihi. Kimsingi, umitindo unaweza kuchunguza mtindo wa kinachosemwa au kuwasilishwa na jinsi kinavyowasilishwa au fani na maudhui. Maelezo haya yake yanakaribiana na yanayotolewa na Njogu (2007) kwamba, kifasihi mtindo huelezwa kwa kuainishwa na madhumuni ya msanii. Madhumuni ni dhamira na mtindo ni jinsi dhamira zinavyowasilishwa. Kauli hii inabainisha kwamba wazo kwanza huota katika fikra za mwanasanaa au msemaji yeyote wa kifasihi. Wadhifa wa mwanasanaa ni kuainisha na kutumia lugha inayofaa kueleza wazo hilo.

Njogu na Chimerah (1999) katika uchanganuzi wao kuhusu mtindo wanasema ni ufundi wa kupanga na kupangua. Pia ni ujuzi wa kujieleza. Wanaendelea kusema kwamba katika kueleza dhana hii, ni muhimu kukumbuka kuwa vipengele vyake ni kama vile: jazanda, taashira, tashbihi, tasfida, taswira, taharuki, mbinu rejeshi, viangaza mbele na kadhalika. Mtindo hutumiwa kupeleka mbele maudhui na dhamira, pamoja na kusanifu kazi nzima, ili ufasaha ujitokeze.

Wamitila (2008) ametubainishia mambo muhimu yanayopaswa kuchunguzwa katika matini au kazi za kifasihi kwa kuegemea katika nadharia ya mitindo. Mambo haya yanahusu vipengele kadhaa. Kwanza, mhakiki wa kazi ya fasihi anapaswa kuzingatia uteuzi wa lugha iliyotumiwa. Hata hivyo suala la uteuzi halihusishwi na maneno peke yake. Huhusishwa na maswala mengine

kama vile: uteuzi wa wahusika, usimulizi, mtazamo wake na wa mada anayoishughulikia. Uteuzi wa kila kipengele kimoja una athari kubwa katika vipengele vingine.

Pili, sarufi huchunguzwa katika uchanganuzi wa mtindo kwa sababu huangaliwa kama msingi mkuu wa lugha ambao unadhibiti matumizi ya lugha yenyewe. Kwa kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu katika kazi za kifasihi, basi sifa na matumizi yake huwa na athari kubwa katika uchanganuzi wa matini za kifasihi. Inawezekana tanzu fulani zikapendelea miundo fulani mahsusi ya kisarufi. Kwa mfano, ushairi unaelekea kupendelea mipinduo ya kisintaksia kwa kiasi kikubwa unapolinganishwa na utanzu wa riwaya.

Tatu, kipengele cha muundo wa kisimulizi au kimatini na usimulizi kinapaswa kuzingatiwa. Kipengele hiki hurejelea matini au utungo wa kisanii ambao anayelengwa anahisi kuwa kuna mabadiliko fulani yanayotokea. Uchunguzi wa muundo wa simulizi unahusika kimsingi na uchunguzi wa msuko wa kazi inayohusika.

Aidha, uchimuzi wa fasihi huweza kuchunguzwa kuambatana na nadharia ya umtindo. Hata hivyo, kimsingi, dhana hii ya uchimuzi inahusishwa na ushairi zaidi kuliko tanzu nyingine. Ingawa hii haina maana kuwa haipatikani kwenye tanzu nyinginezo. Uchimuzi unahusisha sifa za matumizi ya lugha au muundo wa kukiuka sifa za kawaida za matumizi ya lugha. Au kukiuka mpangilio uliozoeleka au unaochukuliwa kama wa kawaida na kaida katika lugha.

Vile vile lugha ya kitamathali na miundo ya lugha huweza kufafanuliwa katika misingi ya nadharia ya mtindo. Lugha ya kitamathali ni sifa muhimu ambayo inapaswa kuchunguzwa katika matini au kazi za fasihi. Uchunguzi huu unapaswa kubainisha umuhimu wa lugha hiyo ya kitamathali katika kazi au matini inayohusika.

Uchunguzi wa lugha ya matini au kazi ya kifasihi unapaswa pia kuchunguza matumizi ya lugha ya picha na huweza kupatikana kwa njia mbili kuu. Yaani, jazanda za kimaelezi (kutokana na maelezo ambayo yanapatikana katika matini fulani) na jazanda za kiishara ambazo si taswira au picha tu bali pia zina ujumbe wa ziada. Kulingana na msingi huu, uchunguzi wa taswira unapaswa kubainisha ni zipi taswira za kijuujuu, zipi zinazorudiwarudiwa, zipi ambazo ni za

kitamathali (zinazohusishwa na tamathali za usemi). Kigezo hiki cha umtindo ndicho kimeongoza uchunguzi wa utafiti wetu.

Pia, mtazamo wa mwandishi kuhusu swala analolieleza huweza kuelezwa kwa kuzingatia nadharia ya mtindo. Mtazamo wa mwandishi huathiriwa kwa kiasi kikubwa na tajiriba ya mwandishi kuhusu maisha au jamii kwa jumla. Mzungumzaji au mwandishi yeyote huuchukua mkabala fulani kuhusu anayoyasema au kuyazungumzia. Mtazamo huo unaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye upokezi wa maneno anayoyasema au jinsi mlengwa anavyoyaelewa au kukipokea kisa kinachosimuliwa.

Kabla ya kuhitimisha maelezo kuhusu nadharia ya mtindo (ambayo tumeitumia katika utafiti wetu) ni vyema kutambua nadharia hii ina historia ndefu inayofungamana na nadharia zingine. Hususan nadharia ya urasimu wa Kigiriki na nadharia ya umuundo. Hivyo basi, tumezigusia kwa muhtasari kwa sababu baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia ya mtindo tuliyoieleza imetokana na nadharia hizi.

Nadharia ya mtindo ina mizizi yake katika wakati wa urasimu wa Kigiriki hususan wakati wa akina Aristotle na Plato. Wana wa wayunani walifunzwa namna ya kutumia lugha ifaavyo wanapojieleza. Burke (2014) anafafanua kuwa mtindo uliotumiwa wa kutumia lugha hususan miongoni mwa walumbi wakati wa urasimu hasa wa Kigiriki ulitegemea hadhira na jambo lililokuwa likizungumzwa.

Mitindo hii ilikuwa imegawika katika vitengo vitatu. Mtindo wa kwanza ulikuwa wa chini ambao ulitumika katika mazungumzo ya kawaida au katika soga. Mtindo wa pili ulikuwa mtindo wa juu uliohusisha maswala mazito. Mtindo huu ulitumia: tamathali za semi, sentensi sahihi kimuundo, uakifishaji unaofaa na kimsingi ulikuwa rasmi. Mtindo huu ulikuwa na ufanisi mkubwa kwa sababu ulifanya wasikilizaji au wasomaji wasisimuke. Mtindo wa mwisho ulikuwa wa kati kati na ulihusisha vipengele vya mtindo wa kati na wa juu. Hivyo basi nadharia ya mtindo imeongozwa na kitengo cha pili cha urasimu wa Kigiriki.

Aidha, Burke (khj.) anadokeza kuwa Aristotle alitoa mchango mkubwa katika kueleza ushairi wakati wa urasimu. Anaeleza kwamba Aristole alijikita katika kufafanua kuhusu umbo la ushairi na jinsi sehemu au viambajengo vya ushairi vinaweza kuainishwa na kueleweka. Alifafanua

kuhusu maswala kama vile uwazi, usahihi, sintaksia na jazanda katika ushairi. Mawazo haya ya Aristotle yalimchochea mwanafunzi wake (Demetrius) kuandika kitabu *On Style*. Demetrius alifafanua aina za mtindo.

Isitoshe, Burke (2014) anasema kuwa vipengele vilivyohusu sarufi ya umtindo wa urasimu vilijikita katika usahihi, uwazi na ufaafu. Usahihi ulihusu sheria za lugha. Uwazi ulimlazimu mwandishi au mwandishi kutumia maneno kama yanavyotumika kila siku. Hivyo basi maneno yaliyo na utata yalipaswa kuepukwa. Tamati, ufaafu ulitumika kueleza matumizi ya lugha yaliyokuwa sahihi kutegemea muktadha mahususi.

Hivyo basi ni dhahiri kuwa wanaurasimu walijikita zaidi katika kueleza mtindo fulani wa lugha ambao ulipaswa kufuatwa ili kueleza jambo fulani. Jambo fulani lilipaswa kuelezwa kwa kutumia mtindo wa lugha uliofahamika. Iwapo swala lilielezwa kwa kutozingatia utaratibu (mtindo) uliofahamika basi yule mtumizi wa lugha alikuwa amepotoka.

Wanaurasimu mkongwe walikuwa wanatumia lugha kueleza mambo yaliyopo katika jamii au kuiga ulimwengu wa binadamu na kisha kuueleza kupitia lugha. Walitenganisha jambo linalosemwa na jinsi linavyosemwa. Hali kadhalika waliangazia zaidi ushairi na hadithi fupi zilioangazia zaidi kuhusu tanzia. Hata hivyo urasimu ulikuwa na manufaa kwa sababu uliwekea msingi nadharia zinginezo kama vile umuundo ambao pia ulichangia ukuaji wa nadharia ya mtindo. Nadharia ambayo imeongoza utafiti wetu.

Baadaye wanaumuundo walichukua usukani wakiongozwa na Roman Jacobson na Victor Shklovsky. Walidhamiria kuboresha dhana zilizokuwa zimeibuliwa wakati wa urasimu. Kimsingi wanamuundo hawa walitaka kufanya uhakiki wa kisayansi wa kifasihi kwa kuchunguza sifa za kiisimu zinazojitokeza katika matini husika.

Mathalan wanamuundo walitaka kuchunguza jinsi sauti, maneno, miundo ya kisarufi kama vile usambamba na ukiushi hufanya utungo ubainike kama shairi. Kwa hivyo walichunguza sifa zilizotumika kutofautisha utungo fulani wa kishairi na usiokuwa wa kishairi. Mathalan, Norgaard na wenzake (2010) wanaporejelea mchango wa Roman Jacobson wanasema kuwa aliangazia jinsi lugha ya kifasihi hasa ukiushi wa kisarufi na usambamba ilivyochimuza moja kwa moja na kujidhihirisha katika ushairi.

Wanamuundo hawa walichochewa na utafiti wa mwanaisimu Ferdinard de Saussure ambaye alijikita katika kueleza muundo unaoweza kutumiwa kueleza lugha zote za ulimwengu. Ferdinard aliibua isitilahi *parole*, *langue* na *langage*. Dhana *langage* alieleza ni mfumo mzima wa lugha au ni lugha ijulikanayo na hutumiwa na wanajamii. *Langue* ni mfumo wa kanuni za lugha husika. Kuhusu *parole* alieleza kuwa ni matumizi ya utaratibu wa lugha ya mzungumzaji binafsi. Ni uteuzi wa kanuni (langue) ambazo msemaji huzitumia katika uandishi au uzungumzaji wake.

Uainisho huu wa Ferdinard ulitumiwa na wanamuundo kuchunguza miundo inayojenga kazi mahususi ya fasihi. Wanamuundo walishikilia msimamo kuwa kazi mbali mbali za fasihi huwa ni mfumo unaojisimamia kama *langage* na una kanuni zake (*langue*) zinazoutambulisha au zinazouweka wazi. Kwa hivyo, wachanganuzi wa kazi ya kifasihi kimuundo wanafaa kuchunguza kanuni za kijumla (bia) za utanzu husika.

Ntarangwi (2004) akifafanua kuhusu umuundo anasema kwamba, ingawa huwa tunatumia lugha kuzungumza kuhusu maisha, Saussure hakulizingatia jambo hilo bali alisisitiza kwamba lugha ni kiungo kamili kinachojisimamia. Kwamba ni kiungo kilicho na masharti na sheria zake. Hivyo basi kuwepo kwa vitu duniani hakuathiri aina ya lugha iliyopo. Isitoshe, alidhamiria kudai kwamba lugha kwa kujisimamia haibadiliki wala vipande vyake haviathiriwi na mabadiliko yoyote ya kijamii.

Kwa maoni yetu, lugha ni mfumo wa ishara nasibu na kila ishara ina sehemu mbili. Kiashiria ambacho ni neno au sauti na kiashiriwa ambacho ni dhana ama kitu mahususi kinachorejelewa. Uhusiano huu ni wa kinasibu; hamna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kiashiria na kiashiriwa. Hata hivyo dhana hizi mbili haziwezi kutenganishwa. Zote ni kama shilingi kwa ya pili.

Wanamuundo walizingatia zaidi viashiria na jinsi vilitumika katika matini kwa kuzingatia sheria zinazotawala matini husika. Yaani wahakiki wanotumia umuundo hutilia maanani sana muundo wa kazi ya fasihi wakipuuza mandhari ya jamii kuhusu kazi hiyo. Walipuuza swala la kuhusisha fasihi na mtunzi wa kazi hiyo ya fasihi. Hali kadhalika walizingatia zaidi utanzu wa ushairi. Upungufu huu wa wanamuundo ulichochea nadharia ya mtindo kuibuka.

Hata hivyo, wanamuundo waliwekea nadharia ya mtindo msingi mzuri kwa maana walichunguza mbinu za kifani. Kwa mfano walieleza kuhusu jazanda, taswira, tashihisi, sitiari, takriri na ukiushi. Walisisitiza kuwa matumizi ya mbinu hizi huipa kazi ya fasihi hadhi hivyo basi kuweza kuitofautisha na matumizi ya lugha ya kawaida.

Kwa maoni yetu mtindo ni jinsi msemaji au mwandishi awasilishavyo kazi yake ili iweze kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia inayovutia. Nadharia hii imetufaa kwa kuwa hujikita katika kuangazia dhima ya kutumia lugha ya kitamathali ya fasihi. Uteuzi wa mbinu hizi za lugha husababisha tofauti kubwa kati ya wasanii na pia katika kule kuwasilisha ujumbe. Mathalani, mtunzi akifanikiwa kutumia taswira vyema bila shaka atafanikiwa kupitisha ujumbe kwa njia rahisi kabisa. Kila neno linalozua taswira huwa na maana na umuhimu hasa kulingana na ilivyotumiwa.

### 1.9 Mbinu za utafiti

#### 1.9.1 Ukusanyaji data

Utafiti huu umefanywa kupitia usomaji wa maktabani. Hii ni mojawapo ya njia kuu za utafiti. Data imekusanywa katika maktaba za vyuo vikuu hususan Chuo Kikuu cha Nairobi (Jomo Kenyatta Library) na Chuo Kikuu cha Kenyatta (Post Modern Library).

Data ya kimsingi tumeipata kwa usomaji mpevu wa *Utendi wa Ngamia na Paa.* Aidha tumepata data ya ngazi ya pili kwa kusoma kwa kina vitabu, tasnifu na machapisho mengine yaliyohusiana na mada yetu. Tulidurusu yale yaliyoandikwa kuhusu mbinu za lugha. Hususan taswira, tashibihi, sitiari na tashititi.

Aidha matumizi ya mitandao yametufaa katika kuchunguza yaliyoandikwa. Katika mitandao hii tumechunguza yaliyoandikwa kuhusu tenzi, mbinu za lugha na nadharia ya umtindo. Hali kadhalika wahadhiri mbali mbali wametufaa kwa kutupa mitazamo tofauti ambayo imetuwezesha kufafanua mada yetu.

### 1.9.2 Uteuzi wa sampuli

Katika utafiti huu njia ya uteuzi wa sampuli imekuwa ya kimakusudi. Uteuzi huu umetuongoza katika kupata data ambayo ni kiwakilishi tosha kilichokidhi malengo ya uchunguzi huu. Katika utafiti huu tumesoma *Utendi wa Ngamia na Paa.* Beti zilizoangazia maelezo yalengayo taswira au zilizokuwa na matumizi ya tashibihi, sitiari, tashititi zimedondolewa. Beti zinazoambatana na utafiti huu zimeteuliwa kimakusudi.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia beti zilizodhihirisha taswira katika *Utendi wa Ngamia na* Paa. Tumezingatia taswira zitokanazo na maelezo ya mandhari, sitiari, tashibihi na tashititi. Pia tumechanganua data kwa kudondoa baadhi ya beti mahususi. Kulingana na utafiti wetu, beti hizi zilikuwa zimetumia maelezo yanayozua taswira mbali mbali kwa kutumia mandhari, tashibihi, sitiari na tashtiti. Aidha, uchanganuzi umezingatia pengo la utafiti na kuongozwa na mihimili ya nadharia ya mtindo.

### 1.9.4 Uwasilishaji matokeo ya data

Matokeo ya uchanganuzi wa data yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Baadhi ya beti zilizogusia taswira, tashibihi, sitiari na tashititi zimenukuliwa. Dhana hizi vilevile zimeelezwa kwa kijumla kisha mifano maridhawa imetolewa kwa kujikita katika *Utendi wa Ngamia na Paa*.

## 1.10 Mbeko za utafiti

Katika utafiti huu, hatukutafiti kwa lengo la kujinufaisha au kuathiri jamii kwa njia hasi. Ili kuinufaisha jamii kwa jumla tumehakikisha kwamba matokeo ya uchunguzi wetu tumeyaweka wazi. Pia, tumejiepusha na uigaji wa moja kwa moja wa kazi za watafiti watangulizi wetu. Ingawa wakati mwingine ilitulazimu kunukuu baadhi ya maelezo ya watafiti mbali mbali ili kufafanua mada yetu kwa uwazi zaidi. Katika mazingira haya, tumefuata kaida za unukuzi. Tumetaja jina la mhakiki au mwandishi na mwaka wa uchapishaji.

### 1.11 Hitimisho

Ili tuweze kufafanua mada yetu kwa njia inayofaa, sura hii tumeiainishwa katika vijisehemu mbali mbali. Kwa mfano, katika usuli wa mada, tumefafanua kwa kijumla kuhusu taswira na matumizi yake katika ushairi na utenzi. Vile vile tumeeleza kwa muhtasari ploti ya *Utendi wa Ngamia na paa.* Aidha, tumefafanua tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu somo na mbinu za utafiti. Pia, katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya mtindo. Nadharia hii imeelezwa kwa kina katika sura hii ili tuweze kufanikiwa katika kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo yetu. Hivyo basi, historia fupi ya nadharia hii imeangaziwa ili kuuwekea utafiti huu msingi mzuri.

## SURA YA PILI

## 2.0 MATUMIZI YA MAELEZO YA MANDHARI KUUNDA TASWIRA KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA*

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeleza dhana ya taswira na dhana ya mandhari. Tumeyachuguza mandhari kwa sababu taswira mbali mbali hazingeweza kuelezeka bila kuyazingatia. *Utendi wa Ngamia na Paa* umefungamana kwa kiasi kikubwa na imani za dini ya Kiislamu. Watafiti wengi wa tenzi za Kiswahili hukubaliana kwamba baada ya majilio ya waarabu katika mwambao wa Afrika Mashariki utunzi na uwasilishaji wa tenzi ulibadilika mara moja. Mathalani, hapo awali tenzi zilikuwa zinahusu maswala ya kawaida kama vile ndoa, vita n.k. Vile vile tenzi hizi zilikuwa zinawasilishwa kwa kughaniwa kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa hivyo, baada ya waarabu kuja, tenzi zilianza kuandikwa kwa hati ya kiarabu na maudhui yakabadilika; yakafungamana na dini ya Kiislamu. Utunzi ulibadilika kwa sababu wengi wa watunzi walikuwa wafuasi wa dini hiyo. Knappert (1967) anatoa mchango wake kwa kusema kuwa tenzi za kale za Kiswahili zilikuwa na fomula ya kuanzia. Katika fomula hii, beti za mwanzo mwanzo zilitaja jina la Mwenyezi Mungu pamoja na sifa zake. Isitoshe, sifa za Mtume Muhammad, aila yake, masahaba na wafuasi zilifafanuliwa.

Aina mbali mbali za taswira zimesawiriwa katika *Utenzi wa Ngamia na Paa*. Tumejadili taswira zinazoegemea katika kuona, kuzungumza na kusikiliza, kuonja na kugusa kwa hadhira. Hata hivyo baadhi ya maelezo tuliyoyadondoa katika kueleza dhana ya taswira yanahusu tamathali za lugha kama vile tashibihi na sitiari. Mbinu hizi tumezichanganua katika sura ya tatu.

### 2.2 Dhana ya taswira

Kwa maoni yetu, taswira ni picha inayojiunda au inayoundwa akilini mwa msomaji, msikilizaji au mtazamaji wa kazi ya fasihi. Kimsingi taswira ni lugha ambayo inachora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara. Aghalabu ujenzi wa taswira huhusisha matumizi ya hisia tofauti tofauti. Binadamu ana hisia mbali mbali kama vile: hisia za kuona, kuguza, kusikia, kunusa na kuonja. Hisia hizi humwezesha msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi kuunda picha akilini ili kufasiri ujumbe wa fasihi anaposoma kazi ya kifasihi. Yaani ahusishe anayosoma na ulimwengu wake halisi aujuao. Kutokana na hisia hizi taswira mbali mbali hujitokeza katika kazi ya fasihi.

Kwa mfano: taswira za kuoana, taswira za kugusa, taswira za kusikia, taswira za kunusa, taswira za kuonja n.k.

Taswira huwa inatoa hadhira kutoka ulimwengu wa ubunifu wa mtunzi hadi ulimwengu wa uhalisia. Kwa mfano, mtunzi fulani wa kazi ya fasihi anapotaka kuchochea hadhira yake ichukie baadhi ya matendo ya wanajamii ataumba mazingira yatakayofanya ile hadhira ichukie ile hali. Mathalani, katika hadithi fupi ya *Tumbo lisiloshiba* (2016) mwandishi anatuchochea tuchukie tabia ya ulafi katika jamii kwa kutumia taswira ya jitu nene linalofyeka chakula chote katika mkahawa mshenzi wa Mzee Mago. Jitu hili halikubakisha hata kidogo cha sadaka ya mwenye njaa. Lilipomaliza kukila kile chakula, lilitoa bweu lilokuwa na uvundo wa myama aliyeoza licha ya kuwa lilikuwa limevila vyakula vyenye harufu nzuri kama vile: wali wa nazi, mchuzi wa nyama na nyama ya kuchoma.

Isitoshe, taswira ni fumbo. Kwa hivyo, msanii wa kazi ya fasihi uumba mandhari yaliyo na vitu ambavyo vipo katika hali halisi au vya kufikirika. Jambo hili kumfanya msomaji au msikilizaji atumie hisia zake kuumba picha itakayomwezesha kutambua ujumbe uliofichika. Picha hii aghalabu huacha athari ambayo msikilizaji au msomaji ataikubuka kwa muda mrefu. Mathalani, katika mfano tulioutoa kutoka hadithi ya *Tumbo Lisiloshiba* (khj.*)* ni dhahiri kuwa mwandishi alikuwa anataka tufumbue fumbo kwamba tamaa haifai. Ametumia hisi zetu za kuonja na za kunusa vyakula vizuri kama vile wali wa nazi, mchuzi wa nyama n.k. Kuonyesha kwamba japokuwa jitu lilikula vyakula vitamu liliishia kutoa harufu mbaya ya mnyama aliyeoza kwa sababu lilikuwa linataka kila kitu kiwe chake.

Msokile (1993) anafafanua dhana hii ya taswira kwa kusema kuwa ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake ya fasihi. Katika fasihi, taswira kwa kawaida hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, hasa za sitiari na tashibiha na ishara mbali mbali zenye kuhusu mawazo, dhana, vitu na umbile. Ujenzi wa taswira humfanya msomaji apate aina mbali mbali za hisi zinazoshughulikiwa na kazi ihusikayo ya kifasihi: yaani hisi za kunusa, kuona, kugusa, kuonja na kusikia. Katika hadithi, taswira hujengwa mara kwa mara hasa katika kuelezea mandhari ya matukio yanayoelezwa.

Mohamed (1995) anasema kuwa katika mbinu hii ya matumizi ya picha tunagundua kwamba mwandishi huanza kwa neno au tamko fulani ambalo tayari lina maana fulani katika Kiswahili

neno au tamko hilo baadaye hupewa maana nyingine kwa mbinu ya uhusiano. Yaani mbinu ya kiistiari na baadaye sitiari hizi hukamatana pamoja kuunda picha fulani ambayo huwa ya mashiko au ya hisia au ya zote pamoja.

Mohamed (khj.) anadhihirisha umuhimu wa kuibua hisia katika kazi ya kifasihi. Anasema kuwa lengo mojawapo la mwandishi pengine si kumteka msomaji wake kwa fani na mawazo tu, bali kwa hisia pia; iwe ya furaha, huzuni, ari, majuto na kadhalika. Mwandishi mzuri huweza kuifinyanga lugha mpaka akaweza kumfanya msomaji anacheka ovyo, au anatokwa na machozi au analaani anapokuwa anasoma kazi yake. Hisia za mchanganyiko zinajengwa kwa uteuzi mzuri wa maneno na kwa mjengo wa picha.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kwamba taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji baada ya kusoma, kuona au kusikiliza kazi ya fasihi. Picha hizi huwa zina funzo fulani. Ili kujenga taswira, mtunzi mara nyingi hutumia tamathali mbili za usemi. Jazanda na tashbihi. Wanatoa mfano ufuatao ili kudhibitisha maelezo yao; tusemapo “Kongowea alifanya kazi kama mtumwa’ tunapata taswira ya mtu asiyepumzika wala kupata starehe. Pia tunapata taswira ya mtu anayefanya kazi ya sulubu na anayeteswa kila uchao.

King’ei na Kemoli (2001) wanaeleza kwamba taswira ni mfanano wa vielelezo vya kifikira vinavyoundika akilini kutokana na maelezo fulani katika shairi. Kama sheria mashairi mara nyingi huunda taswira kutupa sisi picha kamili za kimawazo za yale yanayosimuliwa. Picha hizi huweza kufafanua tukio, hali fulani ya mhusika au kisa fulani. Taswira katika ushairi wa Kiswahili na mifano tumbitumbi ya matumizi sio kufafanua maudhui ya shairi tu bali pia na kuonyesha mshabaha kati ya ukweli fulani wa maisha na picha ipatikanayo.

Wamitila (2003) anasema kwamba taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za ki-ishara. Taswira huweza kuundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashibihi na sitiari.

Ntarangwi (2004) anaeleza kuwa taswira ni picha zinazoundwa akilini mwa msomaji kutokana na maelezo ya mtunzi. Ni ile hali ya mtunzi kueleza jambo au kitu fulani wasomaji wake

wakakiona kwa uhalisia kabisa lakini katika akili zao. Kama anazungumzia mahali, wale wasomaji wake wanajenga picha ya mahali pale kiasi cha kwamba ni sawa na kushuhudia mahali pale katika hali halisi.

**2.3 Dhana ya mandhari**

Mandhari ni dhana inayorejelea mahali au sehemu ambayo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itatendeka. Pia hurejelea kipindi au wakati wa kazi ya fasihi. Kwa mfano, kazi za kifasihi zilizoandikwa wakati wa ukoloni au baada ya ukoloni. Katika ushairi tunaweza kurejelea ushairi wa kale hususan tenzi na ushairi wa kisasa hasa ushairi huru. Katika utafiti wetu tumejikita katika kuchanganua taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa* ambao ni utenzi mojawapo wa tenzi za kale zilizohaririwa na kutafsiriwa na Allen (1971).

Mandhari ni mazingira ya kazi ya fasihi. Mandhari yanaweza kuwa ya kiuhalisia au ya kidhahania. Mandhari ya kiuhalisia yanahusu mahali pa kawaida ambapo watu wanaweza kupatambua. Mandhari ya kidhahania yanahusu mazingira yasiyo ya kawaida au yasipo katika ulimwengu wa kawaida. Mandhari haya huwa ya kufikiriwa tu. Kwa mfano, katika *Utendi wa Ngamia na paa* mandhari ya kiuhalisia yanajitokeza msikitini. Katika riwaya ya *Kusadikika* Shaaban Robert (1951) ameumba mandhari dhahania kwa sababu anaunda nchi ambayo inaelea angani.

Ntarangwi (2004) anatoa kauli kwamba ili kazi yoyote ya fasihi ieleweke na iwe ya kuvutia, haina budi kuwa na nguzo au msingi inamokulia. Kwa vile yaaminika kazi ya fasihi huwa inamulika uhalisia wa aina fulani, basi bila shaka lazima iwe na ulimwengu wake. Aghalabu, mandhari huwa kigezo muhimu cha kuielewa kazi ya fasihi. Jinzi mtunzi anavyojenga mandhari yake ni jambo linalosaidia katika kuelekeza msomaji katika kuelewa kazi hiyo zaidi. Kwa kawaida, mandhari ni sura ya mahali hususan jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Kwa mujibu wa Wamitila (2008) mandhari hurejelea mazingira au wakati unaodokezwa na ambao ni msingi wa kazi au kisa kinachosimuliwa.

Ni muhimu kutambua kuwa uteuzi wa mandhari haufanyiki kiholela. Hivyo basi mandhari yana umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi kwa sababu zifuatazo. Kwanza, huchangia ujenzi wa viambajengo vingine vinavyojenga kazi ya fasihi kama vile taswira. Taswira hizi nazo huweza

kuchangia ujenzi wa uhusika au sifa za mhusika fulani. Kimsingi, mandhari hutumika katika kufasiri ujumbe wa kazi ya fasihi.

Pili mandhari huwezesha ujenzi wa mgogoro katika kazi ya fasihi. Mgogoro huu unaweza kutokea baina ya wahusika waliopo katika mandhari yale yale au katika mandhari tofauti tofauti. Migogoro hii ndiyo inayozua maudhui tofauti.

Isitoshe, mandhari yanapaswa kutuwezesha kuhisi au kuona na kupata tajiriba ya yale mwandishi anayotaka tuweze kuyapata katika ulimwengu halisi. Maana ulimwengu wa fasihi ni wa kubuni. Kwa hivyo, mwandishi anapotumia mandhari fulani huwa ametutoa katika ulimwengu wa kiubunifu hadi ulimwengu wa kiuhalisia. Mandhari haya husaidia hadhira ya kazi ya fasihi kuchora akilini picha halisi zinazohusiana na kazi ya mtunzi. Swala hili ndilo limetupa mshawasha wa kuchunguza jinsi mandhari mbali mbali yanavyotumiwa katika *Utendi wa Ngamia na Paa* kujenga taswira mbali mbali.

### 2.4 Aina za taswira

#### 2.4.1 Taswira za kuonekana

Hizi ni taswira zinazochochewa na uwezo wa hadhira wa kutumia macho. Aghalabu huwa zinatokana na mazingira yanayozunguka hadhira au mandhari yanayoweza kuonekana. Mara nyingi, taswira hizi hazina utata kwa kuwa takriban kila mtu huzifahamu, huziona na utagusana nazo kila siku kwa vile zipo katika mazingira yake. Momanyi (1991) anasema kuwa inaaminika kuwa msanii kama mwanajamii huandika kutokana na tajriba anayoipata katika jamii yake.

Taswira hizi za kuonekana Nzilu (2018) anaziita taswira za maono na anasema ni taswira zinazotoa picha inayoonekana wazi wakati msomaji anapitia kazi fulani. Picha hizi ndizo zinazomfanya msomaji alinganishe matukio yanayochorwa akilini na matukio anayoyaona kwenye maisha yake.

Mtunzi wa *Utendi wa Ngamia na Paa* ametumia taswira hii kwa wingi. Tunaweza kuunda picha mbali mbali akilini mwetu huku tukizihusisha na maelezo yanayohusu maumbile tuyaonayo katika ulimwengu halisi au wa kufikirika. Mathalani, ili kusisitiza upekee wa Mtume Muhammad wakati wa kuumbwa kwake, anatueleza maumbile tofauti ambayo hayakuwepo

wakati Mtume Muhammad alipokuwa akiumbwa. Hivyo basi amerejelea mandhari ya kiwakati kumwinua Muhammad na kumpa hadhi zaidi ya viumbe vyote.

Kwa kutumia mandhari ya kiwakati, Muhammad alikuwa kiumbe wa kwanza kuumbwa. Uwepo wake unazidi maumbile ambayo huwa tunafikiri yana sifa za kustaajabisha na zenye upekee. Kwa mfano, katika ubeti wa 13 na 14 tunaelezwa kwamba, ingawa alikuwa amefunikwa baada ya kuumbwa nuru iliyotoka mwilini mwake ilizidi ya mwezi na jua. Hivyo basi, kwa kuwa huwa tunaona nuru ya mwezi na jua tunaweza kufahamu, kwa nini baadhi ya wanajamii humuenzi Muhammad maana nuru yake ilijitokeza kabla ya vitu hivi viwili kuumbwa. Beti zifuatazo zinathibitisha maelezo haya.

uumbilwe mdathini
ikimzagaa nuru
galulati igamaru
wa gabula shamusiya (ubeti wa 13)

uumbilwe muombezi
kusi yuwa kusi mwezi
kusi kiza kivumbizi
na ambapo paangaa (ubeti wa 14)

Taswira mbalimbali za mandhari tofauti tofauti yanayoonekana zinaendelea kudhihirika wazi wazi katika ubeti wa 15, 16, 18, 19 na 20. Mtunzi anaendelea kutueleza kwamba Muhammad aliumbwa wakati hamkuwa: mbingu, nchi kavu, ndege, binadamu, wanyama, maji ya baharini, nyota, moto, simba, ndovu, vitu vinavyosababisha kuwe na kivuli na wanyama wanaotambaa. Vitu hivi vyote vinapatikana katika mazingira halisi ya binadamu. Ubeti ufuatao unadhihirisha maelezo yetu.

kusi nyama hayawani
kusi mai baharini
kusi malaika mbinguni
kusi nyota za kuwa (ubeti wa 16)

Vitu hivi vilivyoteuliwa na mwandishi wa utenzi huu vina umuhimu mkubwa katika mandhari ya kawaida ya binadamu. Hali kadhalika hutumiwa kuashiria taswira mbali mbali katika jamii au

katika fasihi. Kwa mfano, katika hurafa nyingi za kiafirika simba na ndovu hutumiwa kuwakilisha ama kutuchorea picha ya mhusika aliye na nguvu.

Taswira ya kuonekana imekuwa nyenzo kuu ya kuthibitisha mateso ya Ngamia. Wakati Ali alitumwa na Muhammad akachunguze sauti iliyokuwa ikimwita. Ali alimwona Ngamia ambaye alikuwa amesimama huku akilia. Ngozi yake ilikuwa imedhoofika huku mifupa ikidhihiri. Aidha macho yake yalidhihirisha uchovu huku machozi yakitiririka. Wajihi wa Ngamia unadhihirishwa katika ubeti wa 98 na 99. Hatua ya Ngamia ya kuja pale msikitini ni dhihirisho tosha kuwa Ngamia alifahamu kuwa msikitini angepata usaidizi au utulivu. Kinyume na ilivyokuwa katika mandhari aliyokuwa akifanya kazi.

Kama tulivyoeleza hapo awali, mandhari yaliyojitokeza katika utendi huu yamefungamana na dini ya Kiislamu. Kazi mbali mbali za dini ya Kiislamu zimeeleza jinsi wanyama wanapaswa kushughulikiwa. Hususan *Hadith* na kitabu kitakatifu *Quran*. Mathalan, Shirazi (2005) anaeleza kwamba kuna haki sita ambazo wanyama wanapaswa kuwa nazo kwa mujibu wa dini ya Kiislamu.

Haki hizi ni kama vile: wapewe haki ya kulishwa. Pili, wakati wanyama wanapopitia mahali palipo na maji waruhusiwe kuyanywa. Tatu, wasibebeshwe mizigo kupita kiasi wabebe mizigo kifu yao. Nne, hawafai kuchapwa hasa nyusoni kwa kuwa huwa wanamtukuza Mungu. Isitoshe, iwapo itabidi wachapwe hasa wanapokuwa wanafundishwa kutekeleza baadhi ya kazi za kumsaidia binadamu kama vile kubeba mizigo. Anayewafundisha lazima awapige kwa namna inayoonyesha kwamba anajali wale wanyama. Tano, wanyama wasilazimishwe kutembea masafa marefu. Wanaposimama wasilazimishwe kuanza safari; wapewe muda wapumzike. Mwisho wasiwabebe watu kwa muda mrefu na wanapowabeba wasiwapigie makelele.

Katika utendi huu haki hizi za wanyama zimekiukwa. Mwandishi aliwateuwa wanyama wawili; ngamia na paa ili kutuchorea taswira ya jinsi haki za wanyama hawa zinavyokiukwa. Hali kadhalika taswira hizi zinaakisi jinsi binadamu anavyodhulumu binadamu mwenzake.

Sababu kadha zilimsukuma mwandishi kumtumia ngamia. Kwa mfano, ngamia ni mnyama anayeenziwa na jamii nyingi hasa zinazoishi katika maeneo kame hasa ya jangwani. Pili utenzi wenyewe umefungamana na dini ya Kiislamu. Katika *Quran* mnyama huyu ametajwa. Kwa mfano, Barwani (1980) anapoeleza muhtasari wa sura za Quran; katika *Surat Al-Ghaashiyah*

*(88:17)* ametafsiri mstari huu ifuatavyo, "Je! Wanapuuza kuzingatia ishara, basi hebu na wamuangalie ngamia, vipi alivyoumbwa kwa namna ya peke yake kwa uweza wa Mwenyezi Mungu."

Barwani (khj.) ameeleza maumbile mbali mbali ya ngamia yanayodhihirisha utukufu na uwezo wa Mwenyezi Mungu. Amefafanua sifa za ngamia zinazoonekana na zinamfanya awe jahazi la jangwani. Kwa mfano, anasema kwamba macho ya ngamia yamenyanyuka, yanaelekea nyuma na yana kope za kuyakinga na mchanga na vumbi. Vile vile pua na masikio yamefunikwa na nywele kuzuia vumbi. Pia yameumbwa kwa namna maalumu; kunapovuma upepo mkali pua hufunga na masikio hupinda. Miguu ya ngamia ni mirefu na husaidia katika wepesi wa kwenda. Nyayo zake ni pana hivyo basi hutembea juu ya mchanga laini au changarawe bila kutatizika. Aidha chini ya kifua chake na chini ya viungo vyake vya miguu pana ngozi inayofanana na mito. Ngozi hii humwezesha ngamia kupiga magoti na kulala juu ya ardhi ngumu na yenye joto bila ya kudhurika. Pande zote mbili za mkia wake yapo manyoya marefu ya kulinda sehemu za nyuma.

Zaidi ya hayo, amefafanua vipawa mbali mbali alizopewa ngamia kama vile wakati wa baridi hahitaji kuyanywa maji. Vile vile wakati wa kiangazi anaweza kuvumilia kiu kwa muda wa wiki mbili. Katika kipindi hicho hupunguza thuluthi mbili ya uzito wake. Jambo la kwanza linalostaajabisha ni kwamba anywapo maji hurudisha uzito wake wa zamani kwa muda wa dakika chache. Pili, maji ambayo hunywa huwa hayarundiki tumboni kama wafanyavyo wanyama wale wengine. Maji haya huingia katika mfumo wa mwili wa ngamia na huyatumia kwa uangalifu. Hali kadhalika, jasho linalotoka katika ngozi ya ngamia huwa dogo jambo hili husaidia ngamia asipoteze maji aliyoyahifadhi kwa kasi. Pia huhifadhi mafuta katika nundu yanayotumika kufidia ukosefu wa chakula.

Kutokana na sifa hizi mbali mbali za ngamia tumebaini kuwa ngamia ni mnyama wa tunu na hafai kuteswa hata kidogo. Hivyo basi mwandishi wa *Utendi wa Ngamia na Paa* amefanikiwa kutuchorea picha inayonata akilini. Taswira hii imetufanya tuchukie matendo ya Abu Masud ambaye ni kiwakilishi cha wanadamu waovu wanaolipa kazi nzuri kwa madhila.

Ngamia ametumiwa kuakisi unyama wa Abu Masud. Taswira ya kuonekana imetumiwa wazi wazi ili kueleza mtafaruku uliotokea kati ya ngamia na bwana wake (Bwana Abu Masud). Aidha taswira hii ya kuonekana imethibitisha kwa uwazi zaidi jinsi haki za Ngamia zilivyokiukwa.

Ngamia anaeleza kwamba hapo awali alikuwa anabeba mzigo unaopaswa kubebwa na ngamia wawili. Hata hivyo aliweza kuubeba na hata kuwapiku ngamia wale wengine. Siku zote ndiye alikuwa mshindi. Hivyo basi akawa ndiye kiongozi wao.

Siku iliyotangulia alibebeshwa mzigo ambao ulikuwa mzito zaidi. Ilibidi ang'ang'ane sana kuubeba kwa hivyo alianguka mara zaidi ya tisa huku Bwana Masud akimwangalia. Mara ya kumi hakuweza kuamka na wakati uo huo akiwa amepiga magoti Bwana Masud alimpiga na akaendelea kumpiga. Yule Ngamia alijikaza mpaka akafika nyumbani. Bwana Masud alimtua ule mzigo kisha akamfunga kabisa bila huruma badala ya kumwachilia apumzike kutokana na adha alizokuwa amepitia. Maelezo haya yanawekwa bayana katika beti za 120, 121, 125 na 126. Hususan ubeti ufuatao unaakisi yale Ngamia aliyoyapitia.

kwa kuchoka na uzele
nisiweze kwenda mbele
kanguka nazo vivile
naye kinishuhudiya (ubeti 120)

Taswira nyingine ya kuonekana inayofungamana na mandhari inadhihirika njiani. Muhammad, masahaba wake na Bwana Masud walipokuwa wakiandamana kuelekea palipokuwa Ngamia ili kuthibitisha masuala ambayo Mtume alikuwa amemwarifu Bwana Masud. Wanamwona Paa aliyekuwa amefungiwa kirimbani. Paa alipomtazama Muhammad aliinama ili kunyenyekea. Tendo hili linadhihirisha kuwa hata wanyama wanaweza kumtambua Muhammad wamwonapo. Kama inavyojitokeza katika ubeti ufuatao.

paa akita nadhari
ulimuene bashiri
katii yake amri
pamwe na kunyenyekeya. (ubeti  201)

Vile vile yule Paa alikuwa amefungiwa kinyume na haki za wanyama kwa mujibu wa dini ya Kiislamu. Shirazi (2005) anasema kwamba wanyama wanapaswa kuonewa huruma na kuonyeshwa upendo kwani anayewaonea huruma ataonewa huruma wakati wa kiyama. Katika

*Hadith* mojawapo Shirazi (khj.) anaeleza kwamba, Mtume hakuwa pamoja na Masahaba wake. Kisha wale masahaba wakawakamata makinda wawili. Yule ndege mlezi wa wale makinda alihatarisha maisha yake kwa kuwafuata wanawe huku akitoa sauti ya uchungu. Mtume aliporudi na kumpata yule ndege akilalamika aliwamuru warudishe wale makinda mara moja kwani ahurumiaye viumbe wote hata yeye atahurumiwa. Hadithi hii inashabihiana na ya Paa kwa sababu Paa alikuwa na wanawe wachanga aliokuwa amewaacha msituni.

Paa aliwahadithia jinsi alivyoangukia mtego ule. Anatumia taswira ya kuona kuthibitisha madhila anayoyapitia. Mathalani anasema kwamba hana ngozi wala nyama amesalia mifupa tu na huwa anayumbayumba anapotembea. Zaidi ya hayo alikuwa amejifungua wakati alipotekwa nyara na akawaacha wanawe wakitesekea msituni bila chakula.

Taswira nyingine ya kuonekana imedhihirika wakati Muhammad anauliza kuhusu aliyemteka yule Paa. Kijakazi mmoja anayeitwa Taangazi anajitokeza kutoka hemani. Wakati uo huo alipomwona Mtume alimtambua na kukariri shahada mara moja kuwa hamna Mungu mwingine ila Illahu (Allah) na Muhammadi ndiye Mtume (Rasuli). Kwa mjibu wa Ahmad (2000) shahada ni nguzo ya kwanza katika dini ya Kiislamu. Shahada hujenga imani ya dini ya Kiislamu. Shahada ina umuhimu mkubwa kwa sababu hudhihirisha kuwa duniani hamna Mungu mwingine anayepaswa kuabudiwa ila Allah. Pia shahada hudhihirisha kuwa Mtume Muhammad ndiye mtume wa mwisho na aliyekuja kuongoza binadamu katika njia inayofaa. Ubeti ufuatao unaangazia jinsi Taangazi alivyokariri shahada mbele ya mtume na masahaba wengine.

> la illaha ila llahu
> muhamadi rasulubu
> la ghairu siwa llahu
> mpasa kuabudiwa.( ubeti 237)

Pia kupitia taswira ya kuonekana, Mtume Muhammad ameweza kufikia azma yake ya kumkomboa kafiri aliyemteka paa. Wakati Paa aliporudi baada ya kupewa ruhusa na Muhammad akanyonyeshe wanawe msituni. Kafiri aliyemteka Paa alidhania Paa hatarudi. Hata alianza kumkejeli Muhammad akimwambia kuwa Paa hawezi akarudi kwani amerudi katika makao yake ya mwituni. Wakati huo Kafiri akamwona Paa akija kisha akashuhudia Paa akimwinamia Muhammad. Pia alimsikia Paa akimsujudu Muhammad na kumwabudu Mungu (Allah). Kitendo

hiki kilichoshuhudiwa na yule Kafiri kilimfanya abadili azma yake ya kumfungia Paa. Baadaye, yule Kafiri alimwarifu Muhammad atamuachilia Paa arudi palipo na wanawe.

Pengo lililoachwa baada ya kifo cha Muhammad linadhihirika kwa kutumia taswira ya kuonekana. Mathalan, baada ya Ali Masud kukumbali makosa yake na kubadilika na kuwa mwisilamu. Alimpa Ngamia uhuru wa kwenda atako. Muhammand naye alimpa eneo la Banni Hajjar liwe makaazi yake. Ngamia alikuwa anaenda Msikitini kila Ijumaa kusali. Wakati Muhammad alipokufa, alienda msikitini kama kawaida siku hiyo alimtafuta Muhammad kila mahali msikitini walakini hakumuona. Aliona tu Ali (babake Hasan) na masahaba wake; ambao walikuwa wakiomboleza kifo cha Muhammad.

Aidha, ili kuonyesha upendo aliokuwa nao kwa Muhamand Ngamia aliweza kwenda kaburini kwa Muhammad. Kupitia taswira ya kuonekana, kila mtu aliweza kuona jinsi Ngamia alivyoomboleza kifo cha Mtume. Ngamia alifika kaburini mwa Mtume akapiga magoti na akajisuguwa mle huku masahaba wakimwangalia.

### 2.4.2 Taswira za maongezi na masikizi/kusikia.

Taswira hizi za masikizi huchochewa na uwezo wa msomaji au msikilizaji kuweza kusikia maelezo fulani. Taswira hii imetumika kwa njia ya kipekee ili kusisitiza maelezo ambayo siyo ya kawaida. Kwa mfano, Mungu anazungumza moja kwa moja na Muhammad. Aidha wahusika mbali mbali walishangaa jinsi wanyama kama vile Ngamia na Paa wanaweza kuzungumza wakitumia lugha ya binadamu. Baada ya kuyasikia maelezo, haya mchakato unaotokea akilini huzua picha mbalimbali kutegemea maelezo. Kawaida, lugha ya mazungumzo huhusishwa na binadamu. Hata hivyo katika fasihi, wanyama hupewa kipawa hiki cha kuzungumza.

Wamitila (2003) amesema kuwa taswira za usikivu ni taswira ambapo msanii anaunda picha ambazo hulenga hisia za kusikia, yaani anajenga picha zinazohusiana na sauti. Nzilu (2018) anaeleza kuwa taswira ya masikizi hutokana na hisia fulani za sauti. Taswira hizi zinapotokea huwa na athari zinazotokana na sauti yenyewe.

Mathalani tumeelezwa kwamba baada ya Mungu kumuumba Mtume, Mungu aliumba roho mbalimbali za wafanyao mema na mabaya. Wakati hizi roho zilipokuja alipo Muumba aliziuliza iwapo zinafahamu (Mungu ni nani, jina lake ni lipi na hufanya nini). Roho hizi hazikuweza

kujibu hata swali moja kwa hivyo kimya kilitawala. Pia mitume wengine kama Nuhu, Musa, Ibrahimu na Issa hawakuweza kujibu maswali ya Muumba. Vile vile binadamu (Adam) alishindwa kuyajibu.

Muhammad pekee ndiye aliweza kuyajibu. Muhammad alimjibu Mungu kuwa Yeye pekee ndiye anayestahili kuabudiwa na hakuna Mungu mwingine. Aliendelea kusema kuwa anakiri kutoka moyoni mwake kuwa hamna miungu mingine inayopaswa kufananishwa naye. Hivyo basi Mungu ndiye Mungu wa miungu yote. Vile vile ndiye muumba wa vitu vyote. Yeye ndiye anayeuwa watu na wakati uo huo ndiye aletaye ufufuo. Sifa za Mungu na umuhimu wa Muhammad katika jamii haungeweza kutambulikana iwapo taswira hii ya maongezi na masikizi haingetumiwa. Taswira hii inajitokeza kutoka ubeti wa 24 hadi ubeti wa 30.

Baada ya Mola kuridhishwa na majibu haya ya Muhammad, alimwambia kuwa amemnyanyua juu ya viumbe vyote na aliumba viumbe vyote kwa ajili yake. Yaani amemtunuku dunia, malaika na paradiso. Hali kadhalika, Mungu alimweleza kuwa amempa mamlaka juu ya vitu vyote alivyoviumba na zaidi ya hayo atakuwa mwombezi wa kila kitu (taswira hii ndiyo ilikuwa nguzo ya imani ya Ngamia na Paa. Wanyama hawa walikuwa na uhakika kuwa Muhammad ataweza kusikiza madhila yao na bila shaka kuwasaidia).

Taswira hii ya maongezi na masikizi inazua shani ya Ngamia kujieleza na kumtambua Muhammad kuwa yeye ndiye Mtume anayeenziwa na Mungu kuliko mitume wengine. Japokuwa hadithi nyingi za fasihi simulizi hutumia wahusika wanyama wanaofanya matendo kama binadamu. Hasusan kipera cha hurafa. Mathalani Njogu na Chimerah (1999) wanasema kwamba hurafa ni hadithi ambazo wanyama wamehusishwa kwa wingi. Wahusika hawa wanyama huwa wamepewa tabia za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na lugha. Ijapokuwa wahusika ni wanyama, mafunzo huwa yanalenga binadamu tu.

Mathalan, katika *Utendi wa Ngamia na Paa* baada ya Mtume na masahaba wake kumaliza kuomba sala za asubuhi aliisikia sauti dhaifu iliyokuwa ikimwita. Alipoangazaangaza mle ndani msikitini hakuona aliyekuwa akimwita kwa hivyo ikambidi amtume Ali akachuguze ni nani aliyemwita. Ali alipotoka nje alimpata Ngamia amesimama langoni mwa msikiti. Ali alimuliza yule Ngamia iwapo ni yeye aliyekuwa akimwita Muhammad huku akitumia lugha ya kibinadamu. Naye Ngamia akamjibu kuwa ndiye aliyemwita Muhammad na angeomba

Muhammad ajitokeze ili amweleze tatizo lake. Vile vile Ngamia aliendelea kummiminia Muhammad sifa tele. Kwa mfano, alisema kuwa Muhammad ni mpokezi wa siri, asiye na doa na ambaye nuru yake inazagaa kama ya taa. Pia anasema kuwa Muhammad ni mtambulikana na wote. Huwa anayajua mambo yote na bila shaka huyaweka wazi mambo yote.

Ali alienda moja kwa moja akamfahamisha Muhammad salamu alizosizikia hazikutolewa na binadamu bali zilitolewa na Ngamia. Yule Ngamia alisisitiza kuwa angependa kuzungumza na Mtume ana kwa ana. Kwa hivyo taswira hii inatusukuma kutaka kujua Ngamia atayasema yepi mengine. Muhammad na masahaba wengine waliondoka wakaenda alipo Ngamia. Kisha Muhammad akamwambia Ngamia kuwa amweleze alilotaka kumweleza na katu asiogope. Ngamia bila kuogopa chochote alimweleza Muhammad jinsi alivyoteswa na bwana wake Abu Masud yaani alimbebesha mizigo mizito na hata akamchapa. Lakini jambo lililomhuzunisha zaidi ni kuwa bwana wake Masud alisema kuwa keshoye atamchinja. Kisha auze nyama yake ili anunue ngamia mwingine anayeweza kubeba mizigo na ambaye hajakonda. Abu Masud alitongoa maelezo haya yote huku yule Ngamia akisikia. Ubeti ufuatao wa 129 na 130 unabainisha uyabisi wa Abu Masud ambaye anazungumza maneno bila kujali hisia za Ngamia.

mekonda hana unono
ha nyama hana subano
na himli ndito mno
hahimiliye kutukuwa (ubeti 129)

uchapo kesho kuzima
nimtinde nuze nyama
ninunuwe alo mwema
ngamiya mwenye mafaa (ubeti 130)

Ngamia ameweza kupata matumaini kutoka kwa Muhammad kupitia taswira hii ya maongezi na kusikiliza. Mathalan Muhammad alimwarifu Ngamia kuwa afurahiye na amshukuru Mungu kwani Mungu aishiye milele atamwokoa. Kisha akamwarifu aende Bani Hajar atamfuata baadaye.

Chuki ya Abu Masuud inadhihirika wazi kwa kutumia taswira hii ya maongezi na masikizi. Mathalan wakati kijakazi wa Ali Masud alipoenda kumweleza Mtume anamwita. Abu alipaasa sauti na akamwambia mfanyakazi wake kwa hasira kuwa asitaje jina la huyo mtu pale kiamboni mwake. Anakiri kuwa, ulimwenguni mzima hamna jina analolichukia kama hilo la Muhammad na hata hangependa kumsikiliza. Aidha alijiuliza maswali kadhaa. Kwa mfano, Mtume anataka nini kutoka kwake na kwa nini anamsumbua wakati wa mapumziko.

Kwa hivyo taswira hii ya masikizi ni muhimu kwa sababu hutuwezesha kupata picha halisi ya hisia za ndani za mhusika fulani. Mathalan kama jinsi tumekwisha tambua Abu anavyodhihirisha chuki aliyo nayo kwa Muhammad. Vile vile hutupunguzia uchovu wa kupata malezo marefu ya moja kwa moja. Aidha taswira hii ni mojawapo ya kiungo muhimu kinachotumika katika kubaini usimulizi wa utenzi .

### 2.4.3 Taswira ya kugusa

Picha zitokanazo na taswira hii huchochewa na uwezo wa mhusika kushika au kugusa kitu au mahali fulani. Wamitila (2003) anaeleza kwamba taswira za mguzo ni taswira ambazo hujenga picha ya kitu thabiti au kitu kinachoweza kugusika. Kinyume chake ni taswira zinazojenga picha dhahania au anbazo haziwezi kugusika bali ni za kuwaza tu.

Mathalan Ngamia anatueleza jinsi alivyonyanyaswa na Masud kwa kumbebesha mzigo mzito. Hakuweza kuumudu kuubeba kama kawaida. Basi aliangukaanguka na uso wake uliweza kugusa changarawe zaidi ya mara kumi huku bwana wake akimwangalia. Jambo hili linapinga mafundisho ya dini ya Kiislamu kama tulivyokwisha tabua. Kwamba, wanyama wasibebeshwe mizigo kupita kiasi na nyuso za wanyama zisidhuriwe kwa sababu humtukuza Mungu.

Aidha ili kusisitiza unyama wa huyu Bwana wakati Ngamia alikuwa amepiga magoti kwa sababu ya kulemewa na ule mzigo, alimpiga (yaani fimbo iligusana na ngozi ya Ngamia). Hali kadhalika, walipofika nyumbani bwana Masud alimfunga bila huruma. Ngozi ya Ngamia iligusana na kamba. Beti zifuatazo zinadhihirisha adha za Ngamia.

kaanguka nazo habibu
mara kumi kwa hisabu
uso wangu na turabu
zikakutana pamoya (ubeti 121)

kenenda kisikitika
hata nyumbani kifika
kanishusha yake tweka
na kunifunga kambaa (ubeti 125)

akanifunga sharifu
rutubu bi ‘ikilifu
na mayowe uliswafu
shuwara kunifungiya (ubeti 126)

Baada ya kusikiliza Ngamia, huruma iliyomfuma Muhammad moyoni inadhihirika kupitia taswira hii ya kugusa. Kwa mfano, alianguka chini na akalia mpaka machozi yakalovya ndevu zake. Vile vile alifanya vivyo hivyo alipomsikiliza paa.

### 2.4.4 Taswira ya kuonja

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa* taswira hii haijatumika sana. Taswira hii hasa huchochewa na uwezo wa kuonja. Aghalabu uhusisha chakula. Maelezo yetu yanaungwa mkono na Wamitila (2003) anapofafanua kwamba taswira za mwonjo ni taswira anbazo hulenga kwenye hisia ya kuonja. Hali hii inaweza kupatikana kwa mfano pale ambapo pana maelezo yanayohususian na chakula.

Tatizo la Paa na unyama wa aliyemwinda unabainika wazi kupitia taswira hii ya kuonja. Mtunzi ametueleza kwamba Paa alikuwa akimlilia Muhammad ili amuokoe kwa sababu alitekwa baada ya kujifungua.Wakati huo alikuwa ameenda msituni kutafuta lishe bora. Anaendelea kueleza kuwa kwa siku nne sasa wanawe hawajanyonya. Beti zifuatazo zinadhihirisha malalamiko ya Paa.

kuzaa kwangu swadiqi
yeo ni ne twaliqi
hawatambui riziqi
hayawi kwangu ziwa (ubeti 210)

nali kati kulishani
ningiyiziye shabukani
ya aduwi aduwani
muabudu wa shibaa (ubeti 212)

### 2.5 Hitimisho

Aina mbalimbali za taswira huingiliana. Mathalani taswira zinazojengwa na hisia za kusikia humfanya msomaji wa kazi ya fasihi kuunda picha nyingine ya kuona. Vile vile tumebaini kuwa mandhari huwa na mchango mkubwa katika kuunda taswira hizi. Picha mbali mbali zinazoundwa huwa ni za vitu vilivyopo katika mazingira halisi au ni dhahania. Aidha, picha hizi hutambuliwa kwa urahisi na jamii husika. Pia taswira hizi huwa ni nyezo muhimu ya kurembesha kazi ya kifasihi.

Taswira hizi zimeweza kufanya utenzi huu uwe na uhalisia zaidi. Msomaji ameweza kujinasibisha au kutambua ujumbe wa mwandishi kwa njia wazi kabisa. Kwa mfano, katika *Utendi wa Ngamia na Paa* mwandishi ameweza kutumia taswira ya maongezi na masikizi kunasa hisia za msomaji. Ngamia na paa wameweza kuhadithia madhila yao wanayoyapitia mikononi mwa watu mbalimbali kuonyesha unyama wa binadamu (matumizi ya uhusika wa ngamia na paa utaelezwa zaidi katika sura ya ne).

## SURA YA TATU

## 3.0 MATUMIZI YA TASHIBIHI NA SITIARI KATIKA UJENZI WA TASWIRA KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA*

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeeleza kuhusu dhana ya tashibihi na sitiari. Hali kadhalika, aina za mbinu hizi zimefafanuliwa. Kimsingi, katika sura hii tumetimiza lengo mojawapo la utafiti wetu. Tumebainisha jinsi mbinu za tashibihi na sitiari zimetumiwa katika kuumba taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Kila ubeti uliotumia mbinu hizi umeangaziwa ili kudhihirisha uamilifu wa mbinu hizi katika ujenzi wa taswira.

### 3.2 Dhana ya tashibihi

Ni tamathali ya usemi inayohusu kulinganisha au kufananisha vitu viwili au zaidi ambavyo ni tofauti. Ulinganisho huu huwa ni wa moja kwa moja na viungo mbali mbali hutumiwa. Maneno kama vile: mithili ya, kama, mfano wa, kuliko, ja n.k. hutumiwa. Tashibihi vile vile ni ulinganisho unaoakisi mfanano wa vitu viwili tofauti. Mfanano huu hujitokeza kwa kutumia viunganishi vilinganishi.

Ulinganisho huu hulenga sura au tabia au hulka. Kwa mfano, tunaposema fulani ni mrefu kama twiga huwa tumelenga sura. Sura ni umbo la mtu au kitu linavyoonekana ana kwa ana. Aidha tunaposema fulani ni mlafi kama fisi huwa tumelenga hulka. Hulka hulenga katika kudhihirisha mazoea ya kitu au mtu ambayo huwa ni kijisehemu cha jinsi mtu au kitu hicho huishi.

Tashibihi zina umuhimu mkubwa katika uwasilishaji wa ujumbe na sio tu katika kazi ya kifasihi bali hata katika soga za kawaida. Mbinu hii kimsingi hutumiwa kuvuta makini ya wasomaji au wasikilizaji. Hivyo basi huwalazimu wasomaji kuchora picha au kunasibisha kinacholinganishwa na tajiriba au uzoefu wa maisha. Jambo hili huchangia katika kumfanya msomaji kuelewa kwa haraka ujumbe unaowasilishwa. Vile vile huchochea mkondo wa kifikira au kufasiri ujumbe wa kifasihi.

Tashibihi zina dhima kuu katika mawasiliano kwa sababu huwasilisha ujumbe kwa haraka. Vile vile huacha athari fulani katika akili ya msikilizaji au msomaji kwa sababu ya picha inayochorwa akilini na tashibihi zile. Kwa mfano, katika kauli; mtoto huyu anatembea pole pole na katika kauli nyingine tuseme mtoto huyu anatembea kama konokono. Kwa maoni yetu, katika kauli ya kwanza ujumbe unaowasilishwa ni chakavu au ni ujumbe ambao una athari dogo. Ilihali katika kauli ya pili kuna athari inayomfuma msomaji moja kwa moja. Kauli hii itamchochea msomaji aweze kupiga picha ya kufungamanisha jinsi mtoto anavyotembea na jinsi mnyama (konokono) atembeavyo kwa kujikokota. Hivyo basi msomaji anaweza kuchukizwa na tabia ya huyu mtoto. Kwa kuwa amefahamu kasi ya mwendo wa yule mtoto (kutembea polepole zaidi).

Aidha tashibihi ni nyenzo muhimu ya kutoa ujumbe kuhusu kitu au jambo ambalo msomaji halijui kuhusu kirejelewa. Kwa mfano, tukisema fulani ni kama mchwa. Sifa za fulani hatuzijui, lakini akilini mwetu tumechora picha ya mchwa. Sifa hizi za mchwa zitatusaidia katika kufahamu sifa za fulani. Maadam tumetagusana na mchwa katika maisha ya kawaida. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa fulani tunayemrejelea hapa huenda ana sifa ya uharibifu kama mchwa. Kwani mchwa ula kila kitu. Au fulani ni mwenye bidii kwa sababu mchwa ni wadudu wanaonasibishwa na tabia ya kutia bidii hasa wakati wanajenga kichuguu.

Mohamed (1995) anasema kwamba tashbihi ni mbinu ya uhusiano na ulinganishi ambapo vitu viwili huhusishwa baina ya neno kama; kama vile useme, mithili ya, mfano wa na kadhalika. Msingi wa tashbihi katika fasihi ni ule ule wa kutafuta namna ya kuweka wazi maana, dhana, picha au hali fulani kwa mujibu wa ulinganifu wa kipicha.

Wamitila (2003) anasema kwamba tashibihi ni misemo ya kilinganishi ambayo hukielekeza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kuikuza sifa yake. Kimsingi, ufanifu wa tashibihi hutegemea msingi wa picha au taswira na sitiari (metaphor) inayofumbatwa na msemo wenyewe. Anaendelea kubainisha kwamba, tunaweza kuziangalia tashibihi kitaaluma kwa njia mbili kuu. Kwanza, kama usemi wa kilinganishi tu ambapo vitu viwili vinalinganishwa. Pili, kama usemi wa kilinganishi ambao unafumbata maana fulani pia, yaani dhima yake haiishii kwenye kulinganisha tu.

Lugwiri (2011) anaeleza kwamba neno tashbiha linatokana na kitenzi shabihi chenye maana ya kufanana na kulingana na au kuwa sawa na. Anaendelelea kutofautisha tashibiha na sitiari. Anasema kwamba, tashibiha hukaribiana na kuhusiana na sitiari kutokana na hali yake ya kulinganisha vitu tofauti kwa misingi ya uhusiano fulani wa kimaana na kimuundo. Hata hivyo, mbinu hizi hutofautiana na kutokuwepo kwa viungo au vilinganishi katika sitiari na kuwepo kwa viungo hivyo katika tashibiha. Anaendelea kueleza kwamba tashbiha huwa ndefu na ulinganishaji wake huwa wa moja kwa moja. Kwa upande mwingine sitiari huwa fupi na ulinganishaji wake huwa si wa moja. Kutokana na hali hii, sitiari hudhihirisha ubunifu wa hali ya juu na huhitaji uwazaji wa kina kwa upande wa hadhira ili kuweza kupata maana lengwa kwa upande mwingine tashbiha hudhihirisha ubunifu wa kiwango cha chini na haihitaji uwazaji wa kina sana ili kupata maana lengwa.

Tambasi (2011) naye ana maelezo yanayokaribiana na ya Mohamed (khj.) kwa sababu anasema kuwa tashbihi ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Vitu hivyo vinalinganishwa kwa kutumia viungo vifuatavyo; kama, mithili ya, fanana na, lingana na, ja, kama vile, sawa na tamthili ya. Mbinu hii inapotumika msomaji huweza kuichora taswira akilini mwake jambo ambalo linarahisisha uelewekaji wa ujumbe.

### 3.2.1 Aina za tashibihi

### 3.2.2 Tashibihi wazi

Hizi ni aina za tashibihi ambazo hujitokeza wazi wazi katika muktadha. Sifa inayorejelewa kati ya kilinganishwa na kilinganishi hujitokeza moja kwa moja. Hivyo basi picha inayochorwa huwa sio ya kukisia kwa sababu sifa mahususi huwa imetajwa. Kwa mfano, tukisema kuwa fulani ni mchafu kama nguruwe. Picha tutakayoichora ni uchafu uliokithiri kutokana na matendo ya huyu fulani. Yaani matendo yake yanazua uchafu jinsi afanyavyo nguruwe.

Katika hadithi fupi ya *Mapenzi ya Kifaurongo* iliyopo katika diwani ya *Tumbo lisiloshiba* (2016) mfano wa tashibihi wazi umebainika. Dennis anaeleza hali ya kutamauka inayowakumba (yeye na wanafunzi wenzake) wakiwa katika Chuo Kikuu cha Kivukoni. Hali hii ya kutamauka

imechochewa na kutoelewa wanayofunzwa na Dkt.Mabonga. Anasema,"Tunategemea kuwa akilijibu swali hili tutajua dhima hii ya fasihi. Lakini sasa...sasa anaanza kututamkia maneno machungu kama shubiri."

### 3.2.3 Tashibihi funge

Aina hizi za tashibihi humchochea msomaji arejelee muktadha wa matumizi ya tashibihi kwa sababu kilinganishi kilichotumiwa huwa na maana zaidi ya moja. Kwa mfano, tukitumia mfano wetu tulioutumia katika tashibihi wazi tunaweza kupata maana mbali mbali kuhusiana na fulani. Ingawa wakati huu tutasema kuwa fulani ni kama nguruwe. Sifa mahususi ya nguruwe tunayotaka kumlinganisha nayo haijatajwa. Katika hali halisi nguruwe ni mnyama aliye na sifa zifuatazo: mchafu, mlafi (hupenda kula kila wakati), mnene na mwenye kelele. Kwa hivyo iwapo muktadha wa matumizi ya tashibihi hii ulikuwa fulani amewanda tutaichukua sifa ya unene wa nguruwe na kufutilia mbali hizo sifa zingine za nguruwe.

Katika hadithi fupi ya *Tumbo lisiloshiba* (2016) tashibihi funge inadhihirika katika hadithi hii. Mathalani, mwandishi anasema, "Jeshi la polisi lilikuwa limeshika hodari mirau na bunduki zao kuwalinda askari wa baraza la mji ambao kama nzige waliporomosha na kumungunya vibanda vya watu wa Madongoporomoka." Kwa hivyo, japokuwa neno wingi na uharibifu halijatumiwa bila shaka tunajijazia kwa kuchora picha ya vitendo (uharibifu) vya askari hawa kwa kuzingatia tabia za nzige. Huku tukiegemea katika muktadha wa hadithi unaohusu uharibifu na wingi wa askari waliokuja kuwafurusha Wanamadongoporomoka kutoka kwenye ardhi yao

### 3.2.4 Tashibihi jozi

Tashibihi jozi ni aina ya tashibihi inayohusisha matumizi ya vilinganishi viwili ambavyo kwa kawaida huwa vinaambatana. Aghalabu nomino mbili huwa zinaambatana katika hali fulani. Kwa mfano, tukisema kuwa mapacha wale ni kama mate na ulimi. Au wao ni kama mtu na kivuli chake. Tunamaanisha kuwa kamwe huwa hawaachani huandamana kila mahali kama jinsi vitu hivi viwili hufanyavyo.

Mfano wa tashibihi jozi unadhihirika katika diwani ya hadithi fupi ya *Tumbo lisiloshiba* (khj.), katika hadithi fupi ya *Mapenzi ya Kifaurongo*. Dennis anasema, "Almuradi masikini na tajiri wametengana kama ardhi na mbingu." Tashibihi hii inatuthibitishia kuwa mwanya uliopo kati ya matabaka haya mawili yaliyopo katika Chuo Kikuu cha Kivukoni hauwezi ukazibika.

### 3.2.5 Aina za tashibihi katika *Utendi wa Ngamia na Paa*

Katika ubeti wa 7 tashibihi funge imetumika. Tashibihi hii imetumika kusisitiza utukufu au upekee wa Mwenyezi Mungu. Ubeti huu unabainisha kuwa ambaye ana uwezo wa kutenda matendo yote ni Mungu. Hali kadhalika hamna miungu mingine, kitu au kiumbe kinachoweza kulinganishwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo tukichora picha ya vitu vyote vilivyopo duniani viwe halisi au dhahania hamna kimoja kinaweza kufananishwa na Mungu. Ubeti ufuatao unathibitisha tashibihi hii.

hayo mtenda ni yeye
haku mwingine ilaye
na mngu kuliko yeye
na sute twafahamiya (ubeti 7)

Nuru ya Mtume Muhammad inalinganishwa na nuru ya taa. Hii ni tashibihi wazi inayotuchorea taswira ya kuona. Tashibihi hii inatuchochea katika kutubainishia utukufu wa Muhammad kwa sababu tunafahamu umuhimu wa taa katika kuiondoa giza. Kwa mfano;

namtaka adhihiri
mukhubiriwa wa siri
muhamadi mutwahari
mwenye nuru kama taa (ubeti 93)

Katika ubeti huu wa 98 Ngamia aliweza kung'amua kuwa Mtume Muhammad alikuwa ametumwa na Mwenyezi Mungu. Kuondoa giza iliyokuwa duniani (maovu). Basi jinsi taa inavyoondoa giza ndivyo mtume anavyoondoa maovu. Kwa kweli katika *Utendi wa Ngamia na Paa* Muhammad ametimiza azma hii kwa sababu amefanikiwa kuwaokoa Ngamia na Paa waliokuwa katika hatari ya kuangamizwa. Hali kadhalika watesi wa hawa wanyama wawili walibadilika na kuwa watu wema kwa hivyo waliona nuru.

Aidha, Paa anatambua umuhimu wa Muhammad katika ulimwengu wa kuleta mwangaza. Anatumia tashibihi wazi inayohusiana na mwangaza kama jinsi Ngamia anavyoitumia. Katika ulinganisho wake anatumia jua na mwezi. Anasema yafuatayo katika ubeti wa 204;

salamu ndako nadhiru
mstawifu wa nuru
mlingana na qamaru
mshabihana na yuwa (ubeti 204)

Nguvu za uovu alizoshindana nazo Mtume Muhammand zinadhihirika kwa kutumia tashibihi wazi. Tashibihi hii inafafanua jinsi Hasidi wa Mtume (aliyekuwa ameteka paa) alivyokuwa na kikosi kikubwa cha watu. Kikosi hiki kilikuwa kikimsaka Muhammad ili wamwangamize. Kikosi hiki cha Mteka paa tunaelezwa kuwa kilikuwa na nguvu mithili ya fahali katika ubeti 251.

Hasidi wa Muhammad anakubali kumwachilia Paa kwa muda lakini Muhammad katika kipindi hicho akawa ndiye dhamana. Kwa hivyo Muhammad akamwachilia Paa lakini akampa masharti ya kurudi. Msharti haya yanasisitizwa kupitia tashibihi jozi ya mshale na upinde. Masharti haya ya Muhammad yanadhihirika katika ubeti wa 285 na 286 ifuatavyo;

akamwambiya ghazali
enda uye tasihili
mfanowe na mithili
kama mvi wenye quwa (ubeti 285)

mfanowe na jinsi
kama mvi wenye kasi
khuruji 'Iqausi
nikeepo niiliya (ubeti 286)

Baada ya Paa kurudi alienda moja kwa moja hadi alipokuwa Muhammand. Paa alikariri sifa za Mungu na za Muhammad. Kila mtu aliyasikia maneno ya Paa. Mathalan, alisisitiza utukufu wa

Mungu kwa kutumia tashibihi funge. Kwa mfano, anasisitiza kwamba hamna kiumbe anayeweza kufananishwa na Mungu. Ubeti ufuatao wa 317 unafafanua hisia hizi za Paa.

naapa kwake rabuka
wahadahu la shirika
umbali kushabihika
na ziumbeze jamiya (ubeti 317)

**3.3 Dhana ya sitiari**

Sitiari ni tamathali ya usemi inayohusu kuhamisha sifa za kitu kimoja kwa kitu kingine. Viunganishi vya ufafanisho kama vile: kama, mfano wa, ja n.k huwa havitumiki. Sitiari huhusisha ufananisho usio wa moja kwa moja. Maadamu kitu fulani huitwa ni kitu kingine. japokuwa hilo sio jina la hicho kinachorejelewa. Hivyo basi humlazimu mtu kuchora picha ya kuhusisha sifa za kilichotajwa au kuhamisha maaana.

Kwa mfano, tukisema Ngina ni Firauni. Ukweli ni kwamba Ngina yu hai lakini ana sifa za huyu kiongozi wa kihisitoria wa Wamisiri ambaye tayari hayupo kwa ulimwengu wa sasa. Kwa hivyo itatulazimu kuchunguza sifa za Firauni na kuzihusisha na za Ngina. Kwa mfano, pengine Ngina hataki kulegeza msimamo wake hata kama hali yake imedorora. Vile vile Firauni wa kihisitoria hakulegeza kamba kuwaachilia wana wa Isiraeli. Ingawa walikubwa na matatizo mbali mbali zaidi ya mara kumi.

Mbinu ya sitiari imeangaziwa kwa kiasi kikubwa na wataalamu mbalimbali. Kwa mfano, Maelezo ya Mohamed (1995) japo yanalenga kubainisha maana ya sitiari katika kazi za nathari maelezo hayo yatatoa mwelekeo katika utafiti huu. Anaeleza kwamba sitiari huonyesha uwezo wa kuifumbata dhana pana (kwa kutumia picha) kwa neno moja au maneno machache. Anaendelea kueleza kwamba (khj.) katika kuunda sitiari, vitu viwili vinawekwa sambamba katika ulinganifu na kutumia sifa au tabia za aina moja.

Kwa kawaida vitu vinavyolinganishwa ni tofauti sana na kila vikiwa na mwanya au tofauti kubwa ni bora zaidi lakini hatimaye vinachangiana sifa au tabia moja. Vile vile Mohamed (khj.) anasema kuwa sitiari huweza kutumika na mwandishi wa nathari kwa kujenga picha za hisia.

Mwandishi katika hali hii huchora picha ya aina moja au picha mbalimbali zenye uchangamano wenye kujaribu kuwakilisha kitu kimoja.

Tambasi (2011) anasema kwamba sitiari hutumika kwa nia ya kulenga hisia za msomaji na kujenga picha fulani akilini mwa binadamu ambaye ni msomaji wa kazi ya kifasihi inayohusika. Sitiari humwezesha msomaji kutafakari kuhusu taswira iliyojengeka akilini na kupata ufahamu wa kina wa wazo ambalo msanii ananuia kupasha hadhira yake. Maelezo haya ni muhimu kwani yanadhirisha kuna uhusiano kati ya ujenzi wa stiari na taswira.

Mathalani, Karanja (2014) ameweza kushughulikia sitiari mbali mbali zinazojitokeza katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* na sitiari hizi zimeweza kubeba taswira mbalimbali. Kwa mfano, Karanja (khj.) anaangazia shairi *Jipu* na anaeleza kwamba katika shairi hili "jipu' lina maana ya uchungu unaokera moyoni ambao ulianza siku nyingi zilizopita na unaendelea kumkera kama jipu (uvimbe) linavyoanza kutunga mwilini na kuendelea kuwa kubwa na kuzidisha uchungu. Kwa mfano, katika ubeti wa nne anaunakili ifuatavyo;

> Si jana wala si juzi lilipoanza tangu
> Ni mingi mno miezi, n'nadhofu hali yangu

Kwa hivyo kutoka ubeti huu taswira za kuona na taswira za kisaikolojia zinaweza kuundwa kwa sababu lile jipu linaweza kuonekana likikua na taswira za hisia zinaundika kwa sababu tunaweza kuunda taswira inayodhihirisha jinsi yule aliye na jipu anakubwa na uchungu.

Karanja (2014) katika shairi *Ukamilifu wa Mja* anasema kwamba shairi zima lina stiari za viungo vya mwili ambavyo vinamwakilisha binadamu. Hili huenda likawa na maana kuwa binadamu huhitaji kushirikiana na wengine ili aweze kufanya kazi kikamilifu, kwani hakuna binadamu anayeweza kutenda mambo yote. Ametoa kazi mbalimbali za viungo hivi kitaswira. Kama vile ulimi na mdomo na kusema kwamba vikisema vinahitaji binadamu anayepumua kupitia pua. Pua hupitisha hewa mwilini ili kila kiungo kiwe hai. Kwa hivyo kitendo cha binadamu cha kupumua hakitoshi. Ushirikiano wa viungo vingine unahitajika ndiposa mja akamilike.

Wamitila (2003) anasema kwamba matumizi ya sitiari yanaweza kuwa yamelenga hisia au fahiwa fulani au kujenga picha au taswira fulani. Kwa mfano, unapomwita mtu fulani nguruwe inawezekana akawa mtu anayehusika na sifa kadha zinazofanana na za mnyama huyo kama ulafi au ukoo (uchafu). Inawezekana pia ikawa hisia zako kwake ni kama hisia ulizo nazo kila umwonapo mnyama huyo.

Lugwiri (2011) anasema kuwa muundo wa kijumla wa sitiari huwa na sehemu tatu: sehemu ya kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi. Kilinganisha huwa ni kitu kinachotumiwa kufananisha na kingine. Kilinganishi ni kitu kinacholinganishwa ilihali msingi ni ile sifa hulka au hali fulani ya kinacholinganishwa.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba sitiari ni mojawapo wa tamathali za kimsingi (pamoja na tashbihi) katika fasihi. Matumizi ya sitiari au lugha ya kisitiari hayotokezi kwa mapana tu katika matini au kazi za kifasihi bali pia katika mazungumzo ya kila siku. Aidha Wamitila(khj.) anafafanua dhana hii ya sitiari kwa kusema kwamba sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi isiyotumia vilinganishi kama, mithili ya, ‘ja’ mfano wa na kadhalika. Aidha ameainisha aina za sitiari kwa kutumia vigezo viwili vikuu yaani aina za kimsingi za sitiari na aina maalum za sitiari. Katika aina za kimsingi za sitiari, ameziainisha zaidi kwa kutumia misingi mitatu ifuatayo.

Msingi wa tafkira au wazo; ambapo anasema kwamba, ingawa kimsingi sitiari zote zinahusisha fikira au uwazaji, atatumia dhana ya tafkira au wazo kurejelea aina ya sitiari ambazo zinachimuza sifa hizo zaidi kuliko sifa za kimuundo. Kuambatana na msingi huu anaainisha sitiari zifuatazo; sitiari kinzani au sitiari ya usemi mpana, sitiari tendi/hai, sitiari fifi/chakavu, sitiari ya usuli/mzizi, sitiari fiche na sitiari ya dhana.

Msingi wa kimuundo. Anaeleza kwamba kigezo kikuu katika uanishaji huu ni mchango wa muundo au sifa za kimuundo katika sitiari zinazozungumziwa. Kwa mujibu wa msingi huu anadondoa sitiari zifuatazo; sitiari radidifu, sitiari mseto, sitiari ya kimuundo, sitiari sahili na sitiari changamano na sitiari ambatani.

Msingi wa mtindo/usemi. Kuhusu msingi huu anasema kwamba unaegemezwa kwenye sifa za usemi au kuangalia mtindo wa matini au kazi kwa upana. Aina za sitiari zinazopatikana katika msingi huu ni kama vile; sitiari kuu, sitiari ya kikaida na sitiari pana.

Katika kigezo cha pili cha kuainisha sitiari (aina maalum za sitiari) anasema kwamba kitengo hiki kinahusisha baadhi ya tamathali ambazo katika mazungumzo au maandishi huelezwa kama aina tofauti za tamathali za usemi, lakini zinaweza kuangaliwa kama aina maalum za sitiari. Kwa mujibu wa Wamitila aina hizi uhusisha; tashhisi, hisimeto, istiari na mbazi. Katika mbazi anazigawa zaidi katika makundi manne ambayo ni mbazi ya ki-Biblia, mbazi ya kimaadili, mbazi ya kifumbo na mbazi ya kibwege. Maelezo haya ya Wamitila yametufaa sana katika kuelewa sitiari na jinsi inavyochangia ujenzi wa taswira.

### 3.3.1 Aina za sitiari katika *Utendi wa Ngamia na Paa*

### 3.3.2 Sitiari sahili

Vitu viwili vinalinganishwa moja kwa moja na maana yake ni wazi. Mara nyingi hujikita katika kulinganisha nomino na nomino. Sifa za kinachorejelewa husabihiana moja kwa moja na kilinganishi. Uhusiano wa kilinganishi na kilinganishwa hauna utata. Kwa mfano, tukisema fulani ni fisi tuna maana ya kuwa fulani ni mwenye tamaa iliyokidhiri.

Wamitila (2008) anasema kuwa sitiari hii huwa na uhusiano mwepesi na rahisi baina ya kilinganishwa na kilinganishi. Kile kilinganishi huwa na maana moja ambayo inahusishwa na kilinganishwa. Yaani ndiyo msingi wa sitiari yenyewe.

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa* sitiari sahili inajitokeza wakati Mungu anazungumza na Mtume Muhammad. Mungu anamwambia Muhammad ndiye mwezi uliokamilika. Hali kadhalika anasema kuwa yeye ndiye nuru na mhifadhi wa siri zisizojulikana. Hivyo basi kwa sababu tunajua jinsi nuru ya mwezi uliokamilika umulika ardhini hata unaweza kuokota sindano ukitumia nuru ya mwezi! Maelezo haya yanahalalisha mtazamo wa wanajamii wa kumtukuza Muhammad kuliko mitume wale wengine. Ubeti wa 37 unadhihirisha sitiari hii;

ndiwe qamari muniri
ndiwe nuru mnawari
ndiwe muyuzi wa siri
watu wasioyauwa ( ubeti 37)

Pia sitiari sahili inajitokeza katika mazungumzo kati ya wana wa Paa na Paa. Wana wa Paa wanaeleza sifa za Mungu. Wanaeleza kwamba Mungu ni huruma na mjuzi wa mambo yote. Hivyo basi, walipokuwa wakimweleza mama yao arudi walijua fika kwamba Mungu atawahurumia na atawarehemu. Ubeti wa 301 unathibitisha maelezo ya wana wa Paa.

mola wetu ni azizi
ni rahimu mteuzi
alimu ni mtangazi
siri zote aziyuwa (ubeti 301)

### 3.3.3 Sitiari tendi

Ni aina ya sitiari ambayo haitumiki kila wakati katika jamii. Aghalabu matumizi yake hayajazoeleka na hata wakati mwingine haijawahi kutumika. Aghalabu sitiari hii huwa imetungwa ili kuambatana na muktadha. Hivyo basi ikitumika katika ule muktadha kuna uwezekano mkubwa isije ikatumika tena.

Kwa mfano, katika *Utendi wa Ngamia na Paa,* Ngamia anasema kwamba hapo awali alikuwa akibeba mzigo wa ngamia wawili. Katika muktadha huu Ngamia anataka tuchore picha ya jinsi alivyokuwa akibeba mizigo mizito. Katika ubeti wa 115 Ngamia anatoa maelezo yafuatayo;

kwa afiya na utoto
salikiyona mazito
ningatukuzwa mapeto
ya ithineni ngamiya (ubeti 115)

Hivyo basi iwapo alikuwa na uwezo wa kubeba mzigo wa ngamia wawili; basi ni rahisi kuchora akilini mzigo uliofanya patokee mtafaruku kati yake na bwana wake. Huenda huu mzigo ulikuwa

ubebwe na ngamia watatu basi! Jambo hili la kubebesha ngamia mzigo mzito zaidi linadhihirisha unyama wa Bwana Masud.

### 3.3.4 Sitiari dhana

Wamitila (2008) anasema kuwa hii ni sitiari ambayo hutokea pale ambapo kitu fulani au kitu kilichoko katika mawanda fulani maalum kinaeleweka kwa kukiweka katika muktadha au mwanda mwingine tofauti. Kwa maoni yetu ni sitiari inayozua maana kwa kuweka kinachorejelewa katika muktadha wa kitu kingine.

Kwa mfano, katika *Utendi wa Ngamia na Paa* kijakazi wa Bwana Masud alipomwangalia Mtume aliona uzuri uliokuwa usoni mwa Muhammad. Hivyo basi neno uzuri hapa ni sitiari dhana kwa sababu inaonyesha ukamilifu wa Mtume. Yaani hata kabla ya Mtume kujieleza, tayari utukufu wake ulikuwa umejidhihirisha usoni mwake. Jambo hili lilimsukuma kijakazi atake kujua jina la aliyekuwa na uso wa aina hii. Ubeti wa 149 unadhihirisha maswali aliyokuwa nayo kijakazi na ndiyo yamezua sitiari dhana;

kumuonakwe rasuli
usowe uli jamali
kamwambiya hunambili
inalo likaneleya (ubeti 149)

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumebaini dhima ya matumizi ya tashibihi na sitiari katika *Utenzi wa Ngamia na Paa*. Katika utenzi huu tashibihi na sitiari zimetumika katika kuumba picha au taswira ambayo imechochea maswala mbali mbali kudhihirika. Mathalani utukufu wa Muhammad umethibitika kupitia mbinu hizi mbili. Muhammad analinganishwa na vitu mbali mbali ambavyo hutoa mwangaza kama vile jua na mwezi.

# SURA YA NNE

## 4.0 MATUMIZI YA TASHTITI KATIKA UJENZI WA TASWIRA KATIKA *UTENDI WA NGAMIA NA PAA*

### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeeleza maana ya tashtiti. Vile vile tumeeleza jinsi tashtiti hutumiwa katika kuchora taswira mbali mbali zinazotumika katika kuwasilisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Pia tumechunguza sifa za tashtiti huku tukifafanua jinsi zimetumika katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.*

### 4.2 Dhana ya tashtiti

Ni mbinu ya fasihi inayohusisha matumizi ya ucheshi, chuku, kinaya au kejeli ili kudhihirisha uozo wa jamii bila ya kuzua chuki au kumuudhi msomaji au msikilizaji. Aghalabu tashtiti hutumiwa kuchora picha katika akili ya hadhira. Hususan kuhusiana na maswala yanayodhihirisha ukatili au unyama, ubinafsi na tamaa ya wanajamii. Mwandishi anayetumia tashtiti huwa ananuia kuirudisha jamii katika hali halisi inayojikita katika maadili ambayo anafikiri jamii imeyakiuka. Hivyo basi, hudhamiria kuungo'a uovu katika jamii au kuufanya ule uovu usisambae kwa kasi katika jamii.

Tashtiti hujikita katika kukosoa kwa kutumia taswira. Jambo lile linalotiwa katika mizani ya tashtiti huwa linakera jamii. Hivyo basi msanii hutumia mbinu hii ili aweze kuunda picha itakayomwezesha kuikosoa jamii kwa njia ya kujenga picha au kwa njia ya uwazi zaidi. Msomaji anaweza kuchora taswira ya maovu yanayotendeka katika jamii ili aweze kuyachukia na kuyarekebisha bila kuzua vurungu.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa tashititi ni mbinu ambapo mwandishi hutumia vichekesho, kinaya na dhihaka kuufichua uovu fulani uliopo katika jamii. Au ujinga ambao umetawala katika jamii kwa njia inayowafanya wasomaji wachukizwe na kukerwa na jinsi yake. Aidha Wamitila (2008) anaeleza kwamba tashtiti huwa na kilengwa chake kikuu ambacho kimsingi kinapaswa kueleweka kiishara. Ingawa tashtiti inaweza kulenga mhusika au mtu binafsi, tabaka la kijamii au asasi za kijamii. Vilengwa hivyo vinapaswa kueleweka katika upana wa kiishara - kama vinavyosimamia jamii pana.

Hali kadhalika isitilahi tashtiti hutumiwa katika fasihi kurejelea aina ya kazi ya fasihi inayotumia mtindo wa kuirekebisha jamii kwa kutumia tashtiti kama nyezo ya kuwasilisha ile kazi. Katika utafiti huu neno hili tashtiti hatujaitumia kama aina ya fasihi ya kitashtiti. Tumeitumia kama mbinu ya fasihi inayonuiwa kujenga taswira ili ujumbe ubainike.

### 4.3 Sifa za tashtiti na matumizi yake katika *Utendi wa Ngamia na Paa*

Kimsingi, sifa kuu ya tashtiti hulenga katika kukosoa kilengwa. Kila jamii ina kaida zake ziwe zimeandikwa au hazijaandikwa zinazopaswa kufuatwa kutegemea jamii husika. Hivyo basi kilengwa ni mhusika au jambo lililokiuka utaratibu wa kaida hizi katika jamii. Mwandishi huandika kazi yake ikilenga kuikosoa jamii kwa kuonyesha jinsi kilengwa kilivyokiuka maadili yanayokubalika katika jamii. Hata hivyo msomaji anapaswa kufahamu kaida hizi zinazotawala jamii husika. Huchora akilini mwake baadhi ya hizi kaida au maadili haya yaliyokiukwa na kilengwa ili tashtiti iwe na athari chanya.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba kinachofanya kilengwa au kishambuliwa kishambuliwe ni kuwa kinaonekana au kuchukuliwa kama kimeenda kinyume na matarajio, kaida au misingi maalum. Inawezekana kudai kuwa kufanikiwa kwa tashtiti kunategemea kuwepo kwa hadhira au msomaji ambaye kwa kiasi fulani anakubaliana na misingi ya shambulio hilo. Au yuko tayari kuiafiki misingi au kaida zinazodokezwa katika kazi hiyo zilizokiukwa.

Mathalani, katika *Utendi wa Ngamia na Paa* mwandishi anadhamirai kuikosea tabia ya wanajamii hasa walivyonavyo au mabwana ya kukosa shukrani kwa watumishi wao. Kwa mfano, mwandishi wa utenzi huu anatuchorea picha ya Ngamia ambaye wakati mmoja alikuwa na nguvu na alifanya kazi kwa bidii. Hata hivyo bwana wake siku moja alimbebesha mizigo kupita kiasi. Anaposhindwa kutembea yule Bwana anampiga. Ngamia anajikakamua anabeba ule mzigo mpaka anafika nyumbani. Baada ya kufika na kutua mzigo, badala apewe mda wa kupumzika bwana wake alimfunga bila huruma. Aidha anasema kuwa atamchinja ili apate hela za kumnunua ngamia mwingine aliye bora.

Misingi iliyotumiwa kukosoa Bwana Abu Masud imejengeka katika imani za dini ya Kiislamu. Katika sura ya pili (tukieleza kuhusu taswira ya kuonekana) tulieleza baadhi ya haki za wanyama ambazo zinapaswa kuzingatiwa kwa mujibu wa *Quran* na *Hadithi*. Bwana Masud alikiuka haki

hizi zote na ndio maana Ngamia anatafuta usaidizi kutoka kwa Muhammad ili amsaidie kutetea haki yake.

Tashtiti husheheni sifa ya kuelekeza na kuleta mabadiliko. Tashtiti humchochea msomaji kuchukizwa na uovu unaonekana na uliopo katika jamii. Hivyo basi msomaji huchukizwa na tabia potovu ya baadhi ya wahusika. Jambo hili huchochea msomaji ahisi umuhimu wa kubadilika. Kwa mfano, Hasidi wa Muhammad aliyeteka Paa alipoona jinsi Paa alivyofuata maagizo ya Muhammad na kurudi haraka aliamua kubadilika. Hususan baada ya kuona jinsi Paa alivyomsujudu Mungu na Muhammad. Japokuwa hapo mwanzo alikuwa anapanga njama ya kumwangamiza Muhammad na hata akaweka kiasi kikubwa cha pesa ili Muhammad angamizwe. Mwanzo Muhammad alipata habari hizi kutoka kwa kijakazi wake Taangazi. Katika ubeti wa 244 Taangazi anamwambia yafuatayo;

metowa ungi wa mali

amewapa marijali

ili yawe bartwili

wapatapo kukuuwa (ubeti 244)

Hali kadhalika ili kudhihirisha hulka ya watu waovu katika jamii mwandishi anatashtiti jinsi wanavyobadili tabia zao kiholela kama kinyonga. Mathalani, Muhammad, masahaba na Bwana Masud walipokuwa wameketi wakimngoja Mteka Paa uso wake ulijaa hasira alipowaona watu langoni pake. Alipobaini kuwa anazungumza na Muhammad alifurahi sana. Japokuwa moyoni mwake alidhamiria kutenda mabaya. Ubeti wa 265 unabainisha matendo ya Hasidi wa Muhammand ifuatavyo;

katabasamu kateka

neno asikufunika

ndani ya moyo haqiqa

dhwana mbovu akatiya (ubeti 265)

Vile vile alimweleza kuwa alikuwa amelipa idadi kubwa ya pesa ili auliwe. Maneno yake yanadhihirika katika ubeti ufuatao wa 267;

niwapele marijali

na ungi mno wa mali

wakupatapo rasuli

duniyani kukwondowa(ubeti 267)

Kisa hiki kinadhihirisha jinsi watu waovu katika jamii hufanya kila jambo ili kuhakisha kuwa watu wema wameondolewa katika jamii. Watu waovu huwa tayari kutoa mali yao ili kuwadhuru waliowema. Hata hivyo, matendo ya watu hawa waovu hushindwa na matendo ya watu wema. Mathalani, Muhammad alijitolea na akawa dhamana ili Paa arudi msituni kuwanyonyesha wanawe. Baada ya Paa kurudi yule Hasidi alibadilisha nia na kumwachilia Paa kwa sababu ya mambo aliyoyashuhudia.

Hali kadhalika, kisa hiki cha Paa kinadhihirisha katika jamii kuna wanajamii ambao huchukua muda mrefu kubadilika. Kwa hivyo tashtiti inapaswa kuendelea kutumiwa ili kuwasukuma wanajamii hawa wabadilike. Kwa mfano, ujinga wa baadhi ya wanajamii wa kushikilia misimamo isiyofaa unadhihirishwa kupitia kwa tashtiti. Bwana Masud anapoulizwa na Muhammad kama ameridhika na aliyoyashuhudia kuhusiana na kisa cha Paa; anasema kuwa bado anahitaji kumuona ngamia wake na lazima ashuhudie akizungumza. Katika ubeti ufuatao wa 330 msimamo wa kijinga wa Bwana Masud unathibitika;

sharuti nimtizame

ngamiya wangu aseme

nili hai nisimeme

masikiyo kisikiya (ubeti 330)

Baada ya Muhammad kugundua kuwa Bwana Masud hayuko tayari kubadilisha msimamo wake wanaendelea na safari hadi alipokuwa Ngamia. Walipofika, Muhammad alimwambia Ngamia aeleze madhila au malalamishi yake kama jinsi alivyomweleza na asihofie jambo lolote. Baada

ya Bwana Masud kusikiza malalamishi ya Ngamia anajikosoa na kusema kuwa hata yeye amekubali Mungu ni mmoja na Muhammad ni Mtume wake. Anaendelea kusema kuwa amekubali Muhammad ndiye Mtume wa kweli na yale anayoyasema ni ya kweli. Hali kadhalika aliwaambia waliokuwa pale wamsikilize huku akikariri shahada (tayari tumekwisha eleza maana ya shahada katika sura ya pili). Mabadiliko haya ya Bwana Masud yanathibitika vyema katika ubeti ufuatao wa 358;

u mtumi kwa haqiqa

mnena kweli sadiqa

na mimi ni kadhalika

qauli nashuhudiya (ubeti 358)

Vile vile ili kudhihirisha mabadiliko ya kweli anasema kuwa malalamishi ya Ngamia yamemfanya awe huru. Pia alisema kuwa anampa yule Ngamia uhuru wa kwenda popote .

Aghalabu matumizi ya tashtiti huambatana na matumizi ya kinaya. Katika akili ya msomaji anaposoma kazi ya fasihi kuna matarajio huwa anatarajia kuyapata katika ile kazi husika. Iwapo haya matarajio yatabadilika au yatakuwa kinyume hasa yanayochora picha hasi akilini mwa msomaji basi yatazua kinaya. Waandishi wanaotumia mbinu ya kitashtiti hutumia nafasi hii ili kuchora picha itakayofanya msomaji achukie ule uovu hivyo basi kumchochea msomaji kubadilika.

Kulingana na Wamitila (2008) anasema kuwa uhusiano uliopo kati ya kinaya ni wa karibu sana. Tashtiti huwa na kaida fulani zilizo bayana: kuhakiki, kukosoa na kufichua hali fulani. Hii ni dhima ambayo inaweza kutekelezwa kwa kiasi kikubwa na kinaya. Ntarangwi (2004) anasema kuwa kinaya ni kusema au kutenda jambo ambalo linatoa maana iliyo kinyume na vile ilivyosemwa au kutendwa.

Mwandishi wa *Utendi wa Ngamia na Paa* anatuchorea picha ya unyama wa binadamu kupitia tashtiti iliyojikita katika kinaya. Kwa mfano, Ngamia anaeleza jinsi tangu zamani alipokuwa akibeba kiasi kikubwa cha mzigo hata mzigo unaoweza kubebwa na ngamia wawili. Kila mara

alitembea haraka hata alipiku ngamia wale wengine. Siku iliyotangulia alibebeshwa mzigo mzito zaidi na aliposhidwa kuubeba alichapwa hata hivyo alijitahidi akafika nyumbani.

Hali kadhalika, Bwana wake alisema kuwa atamchinja ili aweze kupata pesa za kununua ngamia mwingine aliye na nguvu. Kwa hivyo ni matarajio ya msomaji yule Ngamia angepewa muda wa kupumzika. Vile vile Bwana wake angemwonea huruma na imani kwa sababu amekuwa akifanya kazi vizuri, badala yake analipwa kwa madhila. Jambo hili linamchochea msomaji kuhisi uonevu ulioelekezwa kwa Ngamia. Hivyo basi kuchukia tabia hii ya binadamu ya kuwa punda ambaye asante yake ni mateke.

Vile vile, Bwana Masud hakutarajia yale aliyomfanyia Ngamia yawe yanajulikana na Mtume Muhammad. Bwana Masud alishangaa jinsi Muhammad aliweza kumfafanulia ukatili aliouelekeza kwa Ngamia. Kwa mfano, katika ubeti wa 181, 182 na 183 Muhammad anamwambia baadhi ya maneno aliyoyasema kuhusu Ngamia. Kama vile,

kisa mkakutanika
wewe na nduzo haqiqa
mkatenda kumteka
na qauli kumwambiya (ubeti 181)

nyute mambo mkitaya
mchamba huyu ngamiya
medhoofu zake ziya
hahimili kutukuwa (ubeti 182)

ngamiya nilio nao
wote niwafundiyeo

hoyo ndio mui wao

ambao anitukiya (ubeti 183)

Aidha, katika beti hizi tulizozidondoa (ubeti wa 181, 182, 183) zinathibitisha kuwa katika jamii kuna watu huwaona wengine wakitendewa maovu na wananyamaza. Ama wanakosa kuwakosoa ambao wanawatesa badala yake wanajiunga na wanaoendeleza ule ukatili. Mathalani, marafiki wa Masud badala ya kumkosoa kuhusiana na mtazamo hasi aliokuwa nao dhidi ya Ngamia wake, walijiunga naye katika kumchekelea. Pia walipanga namna ya kumwangamiza.

Jambo hili linamkera msomaji kwani ni matarajio yake wanajamii wanapaswa kutekeleza wajibu wa kukosoana. Sio katika kushiriki katika njama ya kuwaangamiza wengine. Mtume Muhammad amekuwa kielelezo chema kwa kuikosoa hali hii. Kwa mfano, baada ya Ngamia kumweleza Muhammad madhila yake alichukua hatua. Aliendа kwa Bwana Masud kuwasilisha malalamishi ya Ngamia.

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa* mwandishi amedhamiria kuikosoa jamii kuhusiana na kiburi kupitia kwa kinaya. Wakati Muhammad alifika nyumbani mwa Abu Masud na kumweleza kuhusu Ngamia wake aliyemtesa, Bwana huyu alimtusi Muhammad na kumwarifu kuwa amegundua Mtume ni mwongo na mjanja. Pia alimweleza kuwa hataendelea kumsikiliza. Ubeti ufuatao wa 189 unathibitisha jinsi Bwana Masud alivyomkaripia Muhammad;

nimekuyuwa haqiqa

u mwongo sina shaka

siwezi kukupulika

manenoyo kusikiya (ubeti 189)

Baadaye, huyu Bwana Masud aliyemtusi Muhammad na kusema ni mwongo anakiri na kusema kuwa Muhammand ndiye Mtume wa kweli. Vile vile hapo mwanzoni alikuwa anasema kuwa hataki kulisikia jina la Muhammad. Hata wakati kijakazi wake alimletea ujumbe kuwa anaitwa

na Muhammad alimpiga. Alibadilika na kusema kuwa amebaini kuwa Mungu ni mmoja na Muhammad ndiye Mtume. Vile vile familia yake yote iliasi ukafikiri wakawa wafuasi wa Mungu.

Aidha, mwandishi anachekelea uovu wa Hasidi wa Muhammad (mteka Paa) wakati alimpata langoni pake. Hakutarajia kumwona Mtume Muhammad langoni pake kwa sababu alikuwa hata amewalipa watu ili wamsake Mtume na kumuua. Hata yeye anathibitisha kuwa amekuwa akimsaka. Katika ubeti wa 268 anasema yafuatayo;

kwangu salina usono

nalikikwavuza mno

bali lizingiye kono

la wewe kuniiliya (ubeti 268)

Vile vile wakati Paa alipewa kibali cha kwenda kuwalisha wanawe kisha arudi, Hasidi anafurahia kwani alidhania Paa hatarudi. Kwa hivyo, alidhania amepata njia rahisi ya kumuua Muhammad. Paa aliporudi alishangaa sana. Aidha, alishuhudia jinsi Paa alivyomsujudu Mungu na Mtume. Jambo hili lilimchochea Hasidi mpaka akamwambia Mtume kuwa amemwachilia paa arudi kuliko wanawe. Ijapokuwa hapo awali alikuwa amemkaripia Muhammadi wakati alipokuwa anamweleza amwachilie yule paa au amuuzie yule paa. Yule Hasidi alimweleza wazi wazi kuwa hatamuuzia yule paa wala hangependa kujihusisha kwa vyovyote vile na Muhammad.

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa* ili mwandishi afanikiwe katika kutuchorea picha halisi ya unyama, ubinafsi na tamaa ya binadamu vyema ametashtiti matendo haya maovu kwa kutumia wahusika wanyama. Katika fasihi, hususan fasihi simulizi hadithi zinazotumia wahusika wanyama katika uwasilishaji wa ujumbe huwa zinaitwa hurafa. Wahusika hawa huwa wanafanya matendo yote kama binadamu. Kwa hivyo ni rahisi kushambulia hasa tabia hasi za kibinadamu kwa kutumia wahusika wanyama.

Njogu na Chimera (2008) wanasema kuwa hurafa ni hadithi ambazo wanyama wamehusishwa kwa wingi. Wahusika hao wanyama huwa wamepewa tabia za kibinadamu, ikiwa ni pamoja na

lugha. Ijapokuwa wahusika ni wanyama mafunzo huwa yanahusu binadamu tu. Wamitila (2008) anasema kuwa hurafa ni mbinu mojawapo hutumiwa katika ukuzaji na uendelezaji wa tashtiti.

Katika jamii nyingi ulimwenguni hususan katika jamii za Kiafrika wahusika wanyama walitumika katika hadithi kwa wingi. Wanyama hawa walichaguliwa kwa uangalifu ili wawasilishe ujumbe uliodhamiriwa kwa haraka. Hali kadhalika, ilikuwa rahisi kushambulia tabia hasi au upugufu wa binadamu kwa kutumia wahusika wanyama bila kuwaudhi. Kwa mfano, mnyama sungura alipotajwa hadhira moja kwa moja ilijua swala linalohusiana na ujanja halitaepukwa.

*Utendi wa Ngamia na Paa* umejikita katika wahusika Ngamia, Paa na wanawe. Wahusika hawa hawakuchaguliwa kiholela. Kwa mjibu wa jamii iliyorejelewa (jamii ya waarabu) Ngamia ni mnyama anayeenziwa kwa sababu ana sifa kadhaa ambazo ni maalum. Kwanza, jamii ya waarabu hujikita zaidi katika biashara kwa hivyo mnyama huyu ni wa manufaa katika usafirishaji wa bidhaa. Pili, eneo la uarabuni ni jangwa kwa hivyo ngamia ndiye mnyama anayeweza kuishi mazingira haya ya jangwani kutokana na maumbile yake. Mathalani ana miguu mirefu inayomwezesha kutembea jangwani. Ana nundu inayomwezesha kumudu kuishi katika mazingira haya bila chakula na maji. Aidha anaweza kujizuia changarawe isimwingie machoni au puani. Vile vile huweza kujikinga kutokana na hali ya anga kama vile joto kali au baridi kali.

Umuhimu wa ngamia na matumizi yake katika kazi ya fasihi haijitokezi tu katika waarabu pekee. Kwa mfano, Abokor (1987) alitathimini jinsi ngamia alitumiwa na watunzi wengi wa mashairi kama ishara ya taifa la Wasomali na uhuru wao kutoka kwa wakoloni. Ngamia alitumiwa kuwakilisha maswala mbali mbali yaliyojitokeza katika jamii hii ya Somali hasa baaada ya kupata uhuru. Kabla ya Abokor (khj.) kutudondolea baadhi ya mashairi yaliyotumia ngamia katika kuwasilisha ujumbe wake anaeleza kwamba Wasomali wanamuenzi ngamia kuliko wanyama wale wengine hasa ngamia wa kike. Ngamia wa kike alipendwa zaidi kwa sababu ana uwezo wa kutoa maziwa mengi zaidi akilinganishwa na wanyama wale wengine. Maziwa ya ngamia huwa hayaharibiki haraka. Pia yakiganda huweza kutumika kwa muda mrefu.

Abokor (khj.) akirejelea shairi lilotungwa na Ali Hussein anasema kwamba wakoloni waliwanyanyasa kwa kuwaulia ngamia wao wa kike. Katika shairi hili ishara ya fisi ilitumiwa

kuwakilisha wakoloni. Anaendelea kusema kuwa hata wao siku moja watafanikiwa kuwauwa wale fisi na kuwaweka ngamia wao wa kike huru.

Aidha, katika shairi lingine la Abdullahi Sultan, Abokor (khj.) anasema kuwa mshairi huyu alichukizwa na hatua ya Uhabeshi kushambulia taifa la Somali baada ya Somali kupata uhuru. Hivyo basi alitunga shairi akilaani kitendo hiki na kusema kuwa uhuru wa Somali ni sawa na wa kukomboa kikundi cha ngamia kilichokuwa kimeibwa na wavamizi. Kwa hivyo kama jinsi ngamia huwa wanalindwa baada ya kukombolewa vivyo hivyo ndivyo watatuza uhuru wao. Walikuwa wanawaonya Wahabeshi kuwa wakiwashambulia tena hata wao watawashambulia kwa jazba.

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa*, Ngamia ametumiwa kuwakilisha hasa wafanyakazi ambao huwafanyia mabwana wao kazi kwa bidii. Licha ya kufanya kazi kwa bidii hudharauliwa au hutendewa unyama. Ngamia ametumiwa kukashifu tabia kadhaa za binadamu ambazo ni hasi. Kwanza, mwandishi anakashifu tabia ya binadamu ya kuwatumikisha wafanyakazi kupita kiasi. Hususan wanapokuwa na nguvu. Wakati nguvu zinapopunguka wanaanza kutafuta jinsi watawafuta kazi au kuwangamiza ili wawajiri wengine walio na nguvu. Mathalani, wakati Ngamia aliposhindwa kuubeba mzigo bwana wake anasema kuwa atamchinja. Kisha auze nyama yake ili apate hela za kununua ngamia mwingine. Licha ya kuwa huyu Ngamia hapo awali alikuwa akibeba mzigo wa ngamia wawili. Kwa mfano, katika ubeti wa 115 na 116 Ngamia anathibitisha bidii aliyokuwa nayo;

kwa afiya na utoto
salikiyona mazito
ningatukuzwa mpeto
ya ithineni ngamiya (ubeti 115)

ingawa na nyingi tweka
nalichenda haraka

na mishindo mwa naka

nyuma sikuonekeya (ubeti116)

Swala hili la kutaka kumchinja Ngamia kwa sababu ameshindwa kubeba mzigo siku moja linaonyesha ubinafsi mkubwa ambao hutawala binadamu. Kwamba hupenda kitu, mtu au jambo linapomfaa. Iwapo halimfai tena ulifutilia mbali.

Aidha, mwandishi anakashifu tabia ya binadamu ya ukatili. Kwa mfano, Bwana Masud alimbebesha Ngamia mzigo mzito na alipotatizika kutembea alimpiga. Licha ya kwamba hapo awali alikuwa anabeba mzigo unaopaswa kubebwa na ngamia wawili. Vile vile alipofika nyumbani badala amwachilie apumzike alimfunga bila huruma.

Pia kupitia kwa Ngamia mwandishi anakashifu tabia ya binadamu ya kuchekelea watu wakati wanakumbwa na matatizo. Au kumkejeli mtu apokabiliana na hali ngumu. Kwa mfano, baada ya Bwana Masud kumfunga Ngamia aliwaeleza ndugu zake huku Ngamia akimsikiliza kwamba hana mafuta wala nyama au nguvu na hawezi akabeba mzigo mzito.

Vile vile mwandishi anaonyesha ujinga unaomgubika binadamu wa kufikiri kwamba anaweza kuthibiti maisha yake na kusahau uwepo wa Mwenyezi Mungu. Mathalan, Mtume anapomweleza Bwana Masud maovu aliyoyaelekeza kwa Ngamia alishangaa. Bwana Masud alishangaa kwa sababu alikuwa amemfungia Ngamia. Zaidi ya hayo, Mtume alipomweleza maelezo hayo yote aliyapata kutoka kwa Ngamia mwenyewe hakusadiki. Hakuelewa Ngamia anawezaje kuwasiliana kwa lugha ya kibinadamu.

Hivyo basi ilibidi waandamane ili Bwana Masud akamsikize Ngamia mwenyewe akieleza madhila aliyomfanyia. Walipofika alipokuwa Ngamia, Masud alishuhudia jinsi Ngamia alivyomsujudu Mungu na Mtume. Jambo hili lilimshangaza Masud mpaka akabadilika. Kwa hivyo, mwandishi anadhamiria kuonyesha jamii ya kibinadamu hata wakikosa kumsujudu Mungu wanyama wanatambua uwepo wa Mungu na bila shaka watamwabudu.

Katika jamii nyingi ulimwenguni paa huwa anahusishwa na sifa ya kuwa mwangalifu. Vile vile ni mwepesi wa kukimbia ili aweze kukabiliana na mahasimu wake kama vile duma au chui. Hali

kadhalika paa hujulikana kama mnyama ambaye ana ufanisi katika maisha yake. Kwa mfano, siku zote huweza kukabiliana na maadui wake ambao wana mbio kumshinda kwa sababu wakati anapokimbia ukimbia kwa kutumia mtindo wa kuyumbayumba au zigizaga ilihali mahasimu wake hutumia mtindo wa mstari wima kwa hivyo mara nyingi huwachanga kiasi ya kwamba hawawezi kumshika. Pia paa hujulikana kama mmojawapo wa wanyama ambao ni warembo duniani.

Katika *Utendi wa Ngamia na Paa*, vile vile Paa ametumiwa kuwakilisha tabia hasi za kibinadamu. Mathalani, aliyemteka Paa alijijali mwenyewe. Alidhihirisha tabia za ubinafsi kwa sababu pengine alimteka Paa yule kwa sababu ya urembo wake. Hakutilia maanani Paa alikuwa na wana wachanga.

Mwandishi anakashifu tabia ya binadamu ya ukatili. Au ya kuwanyanyasa wanyonge. Kwa mfano, aliyemteka Paa alijua kuwa ana wana wadogo lakini hakumhurumia wala kuwahurumia wanawe. Hata wakati Muhammad alimweleza amwachilie yule Paa bado hakupendezwa na pendekezo hilo.

Hali kadhalika mwandishi ametumia wanawe Paa kuwachekelea binadamu hususan wasiotambua uwepo wa mwenyezi Mungu. Wana hawa wa Paa walionyesha ukomavu zaidi wakilinganishwa na Hasidi aliyeonekana kufurahia kitendo cha kumwangamiza Muhammad. Mathalani, Paa aliporuhusiwa aende akawanyonyeshe wanawe; alipofika aliwaeleza kwamba ameruhusiwa aje kuwanyonyesha kwa sababu Mtume ndiye dhamana yake. Baada ya kusikia maelezo hayo walimwambia mama yao arudi mara moja. Wana wa Paa walihofia huenda Muhammad yuko katika hatari ya kuangamizwa na Hasidi kwa hivyo wakamwimiza mama yao arudi mara moja. Hata walishangaa jinsi mama yao aliweza kukubali Mtume Muhammad awe dhamana. Mathalani, beti zifuatazo zinadhihirisha baadhi ya maelezo ya wana wa Paa;

nini mama wetu nini

mtumi kumrahini

huchi aba 'lhasani

humsitahi rasuwa (ubeti 295)

rudi hima ghazilani

kwa ajili dalihini

muhamadi rahanini

ukapate kumtowa (ubeti 299)

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia matumizi ya tashtiti katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Mbinu hii imesawiri taswira ya ukatili, ubinafsi na uovu wa binadamu kwa kijumla. Aidha mwandishi ameweza kufanikiwa katika kuikosoa na kuielekeza jamii. Hususan amefanikiwa katika kusawiri maadili yanayopaswa kufuatwa katika jamii. Hasa yanayojifunga katika kusadiki Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad.

Mtunzi wa *Utendi wa Ngamia na Paa* amefanikiwa kutumia mbinu ya tashtiti katika kurekebisha na kufichua uozo. Mathalani, taswira ya kuonekana inadhihirika baada ya Bwana Masud kubadilika na kuacha unyama wake. Bwana Masud anabadilika na kuwa mwisilamu. Ili kuthibitisha uwajibikaji wake anamweka huru Ngamia. Pia familia yake yote inakuwa miongoni mwa wafuasi wa Muhammad.

SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia muhtasari wa utafiti wetu kuanzia sura ya kwanza hadi ya nne. Aidha sura hii imetumika kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Matokeo haya yameongozwa na malengo ya utafiti wetu kwa kuzingatia msingi wa nadharia ya mtindo. Katika utafiti wetu tumeelekezwa na nadharia hii ya mtindo. Pia katika sura hii tumetoa mapendekezo kwa watafiti wengine.

## 5.2 Muhtasari wa sura

Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya tashibihi, sitiari, tashititi na maelezo ya mandhari katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa*. Tumejadili jinsi mbinu hizi zimetumika katika ujenzi wa taswira. Tumejikita katika malengo ya kubainisha jinsi tashibihi, sitiari, tashititi na maelezo ya mandhari yametumiwa kusuka taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Hatimaye, tumefafanua aina za taswira ambazo zimejitokeza. Malengo haya yamechanganuliwa na kufafanuliwa kwa kuelekezwa na nadharia ya mtindo. Hali kadhalika, malengo haya ya utafiti yametawala sura nne za utafiti huu.

Katika sura ya kwanza tumeangazia usuli wa mada. Katika sura hii tumewekea utafiti wetu msingi kwa kutoa maelezo kuhusu taswira. Tumegusia umuhimu wake katika ushairi na tukadhihirisha jinsi taswira ina dhima kubwa katika kuwasilisha ujumbe wa tenzi.

Pia katika sura hii tumefafanua tatizo la utafiti ambalo limetuongoza katika kuzua maswali ya utafiti. Aidha tumejadili sababu ambazo zimetuchochea kuchagua mada hii ya utafiti. Vile vile katika sura hii ya kwanza tumeeleza upeo na mipaka. Yaliyoandikwa kuhusu somo hayakuwekwa pembeni.

Isitoshe, katika sura hii ya kwanza tumejadili nadharia ya mtindo kwa kina. Nadharia hii ndiyo imekuwa nguzo ya utafiti wetu. Katika kijimada hiki tumeeleza kuhusu waasisi wa nadharia hii na kubainisha wazi mihimili ambayo imefaa utafiti wetu.

Hali kadhalika, tumejadili mbinu za utafiti ambazo tumetumia. Katika kipengele hiki tumejadili kuhusu: ukusanyaji data, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji matokeo ya data. Pia mbeko za utafiti zimejadiliwa kwa kina.

Katika sura ya pili tumeeleza jinsi mandhari mbali mbali yamechochea undaji wa taswira mbali mbali katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Vile vile katika sura hii tumeeleza dhana ya taswira. Tumeangazia maoni ya wataalamu mbali mbali kuhusu taswira. Tumejadili aina za taswira ambazo zimejengwa katika utendi huu na umuhimu wake katika kuwasilisha ujumbe wa utendi huu. Baadhi ya taswira ambazo tumeziangazia ni kama vile: taswira za kuonekana, taswira za maongezi, taswira za kuguza na taswira za kuonja. Kwa kutumia sampuli ya kusudi tumechagua beti ambazo taswira inajengeka kwa kuathiriwa na mandhari mbali mbali.

Tumefafanua nafasi ya tashibihi na sitiari katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa* katika sura ya tatu. Katika sura hii tumeeleza dhana ya tashibihi kwa jumla. Hali kadhalika tumefafanua aina za tashibihi ambazo zimejitokeza katika utenzi huu. Pia tumeeleza zimejenga taswira ya aina gani. Aidha tumeeleza dhana ya sitiari. Tumeangazia jinsi sitiari hutumiwa katika kuumba taswira mbali mbali. Tumethibisha kuwa sitiari hizi humsaidia mtunzi kueleza ujumbe wa utenzi kwa njia inayovutia hisia za wanajamii.

Katika sura ya nne ujenzi wa taswira kupitia mbinu ya tashititi umejadiliwa kwa kina. Sifa za tashtiti zimejadiliwa pamoja na jinsi zinavyochangia ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Sifa hizi zina mchango mkubwa katika ujenzi wa taswira. Kwa mfano, tashtiti hujengwa kwa kutumia kinaya. Hivyo basi, ili kinaya kinachojenga tashtiti kibainike vyema ni lazima taswira mbali mbali zitumiwe.

Kwa mfano katika *Utendi wa Ngamia na Paa* taswira ya kuona inayohusu kumbebesha Ngamia mzigo kupita kiasi na kupigwa anaposhindwa kubeba mizigo inazua kinaya. Ijapokuwa hapo mwanzoni Ngamia yule yule alikuwa akisifika kwa sababu ya umairi wake katika kubeba mizigo. Jambo hili linatuchorea taswira murwa inayokosoa tabia hasi ya binadamu ya kumpenda binadamu mwenzake anapomtumikia; anapokumbwa na changamoto anapomfanyia kazi anamchukia hata bila ya kufikiria nama ya kumsaidia kupambana na changamoto zile. Aghalabu

matatizo haya huwa yamesababishwa na mabwana wenyewe. Mathalani Ngamia anashindwa kubeba mzigo sio kwa sababu ni mzembe lakini alikuwa amebebeshwa kupita kiasi.

### 5.3 Matokeo ya utafiti

Katika utafiti huu tumedhamiria kuthibitisha iwapo aina mbali mbali za taswira ambazo zimetumiwa na mtunzi kama zinafaa. Hali kadhalika tumejikita katika kuchunguza iwapo taswira hizi zinaweza kunasibishwa na ulimwengu halisi hasa uliochota ufananisho kutoka kwa fasihi simulizi. Tumegundua kuwa mwandishi wa utenzi huu amefanikiwa katika kutumia taswira mbali mbali zinazolenga ulimwengu halisi.

Kwa mfano, anapoeleza kuhusu ukatili na tabia ya binadamu ya kukosa shukuran amemtumia mnyama ngamia. Ulimwenguni kote ngamia ni mnyama anayetambulika. Tulijadili sifa maalumu za ngamia zinazofanya kiumbe huyu awe tofauti na wanyama wengine katika sura ya pili. Sifa hizi zimemwezesha mtunzi kuchora taswira mbali mbali ambazo zimebainisha ujumbe wa utenzi huu. Mathalani, kwa kutumia taswira ya kuonekana tunaelezwa jinsi Ngamia aliyekuwa wa manufaa hapo awali anadhulumiwa baada ya kushindwa kubeba mzigo ambao ulikuwa mzito zaidi. Kwa hivyo mwandishi amefanikiwa kunasa hisia za hadhira kwa kushambulia tabia hasi za ukatili wa binadamu mwenzake kwa njia ya mafumbo hivyo basi kuzuia hisia hasi. Yaani mwandishi ameikosoa jamii kwa njia ya upole.

Pia tumedhamiria kueleza aina mbali mbali za taswira ambazo zimejitokeza katika *Utenzi wa Ngamia na Paa*. Ni wazi kuwa taswira mbali mbali zimedhihirika kwa njia ya moja kwa moja. Hivyo basi vimevutia msomaji pamoja na kuleta uhalisia. Kwa mfano kupitia taswira ya maongezi na masikizi wanyama Ngamia na Paa wanampa Muhammad sifa tele. Makafiri kama Ali Masud (bwana wa Ngamia) na aliyeteka Paa wameshindwa kutambua utukufu wa Mungu uliopo kwa Muhammad. Hivyo basi mwandishi ametumia wanyama hawa ili watuchoree picha kamili ya upumbavu wa binadamu kwa njia inayozuia uhasama kuzuka. Hali kadhalika tumebaini kuwa taswira zina umuhimu mkubwa katika kukuza uwasilishaji wa ujumbe. Hasa hudhihirisha hisia za ndani za mtunzi.

## 5.4 Muhtasari wa matokeo

Katika utafiti huu tumebaini kuwa ujenzi mzuri wa taswira ni mbinu nzuri inayotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira yake. Tumegundua kuwa mwandishi ameweza kutumia sitiari, tashibihi, tashtiti na kuzifungamanisha na mandhari. Mbinu hizi zimemwezesha mwandishi kutumia vitu mbali mbali vilivyopo katika mazingira. Vitu hivi ambavyo amevitumia ni halisi au ni dhahania. Vimemwezesha kuunda taswira ambayo inaacha athari fulani ambayo ni nzito katika akili ya hadhira.

Mathalani, tumebaini kuwa ili mwandishi asisitize upekee wa Muhammad ametueleza kuwa Muhammad aliumbwa wakati vitu kama vile mbingu, nchi kavu, ndege, binadamu, wanyama kama vile simba na ndovu hawajaumbwa. Vitu hivi ambavyo mwandishi ameviteua vina umuhimu mkubwa katika mandhari ya kawaida ya binadamu. Kwa mfano, katika fasihi simulizi mnyama simba ananasibishwa na ufalme. Kwa hivyo tunapoelezwa Muhammad aliumbwa kabla ya mnyama huyu ni ishara tosha yeye ni mfalme wa wafalme. Hivyo basi tumebaini kuwa ujenzi ufaao wa taswira umeufanya *Utendi wa Ngamia na Paa* kuwa na uhalisia.

## 5.5 Mapendekezo

Katika utafiti wetu tumeangazia dhima ya tashibihi, sitiari, tashtiti na maelezo ya mandhari katika ujenzi wa taswira katika *Utendi wa Ngamia na Paa.* Ijapokuwa tumeangazia jinsi mbinu hizi zinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi hatujaeleza kwa kina maudhui yanayojitokeza katika utendi huu. Hivyo basi, tunapendekeza utafiti wa kina ufanywe unaohusu maudhui kwani ijapokuwa utendi huu ni wa kale unahusu maswala yaliyopo katika ulimwengu wa sasa kama vile: ukatili, ukiukaji wa haki na ukafiri. Hali kadhalika tumeangazia mbinu chache za lugha. Utendi huu una ukwasi mkubwa wa mbinu zingine za lugha ambazo zinaweza kufanyiwa utafiti.

Aidha, tumeeleza utenzi ni hadithi ndefu ambayo huandikwa kwa njia ya ushairi. Bila shaka hadithi huwasilishwa kwa njia ya masimulizi. Kutokana na ukweli huu tunapendekeza utafiti hufanywe kuhusiana na dhana ya uwasilishaji wa maudhui ya utendi huu. Hususan usimulizi.

# MAREJELEO


Abedi, A. (1954*). Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East African Publishing Bureau.

Abokor, C. A. (1987). *The Camel in Somali Oral Traditions.* Uppsala: Motala Grafiska.

Ahmed, A. (2000). *Why Islam?* Cairo: Islamic inc Publishing & Distribution.

Ahsan, M. (1985). *Islam: Faith and Practice*. Nairobi: Islamic Foundation.

Barwani, S. (1980). *Jifunze Kusoma Kiarabu na Juzuu Amma*. Nairobi: Islamic Foundation.

Burke, M. (2014). *The Routledge Handbook of Stylistics.* New York: Routledge.

Allen, J. W. T. (Mhar.) (1971). *Tendi.* Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

Chokocho, A. na Kayanda, D. (wahar.) (2016). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Crystal, D. na Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Cuddon, J. A. (1997). *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Oxford: Blackwell Publishers.

Husain, A. (1988). *Carmel in Mountains*. Karachi: International Islamic Publishers.

Karanja, M. (2014). *Matumizi ya Istiara, Tashibiha na Taashira Katika Diwani ya Sauti ya Dhiki.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kingei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushahiri.* Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Knappert, J. (1967). *Swahili Islamic poetry*. Leiden: E.J. Brill

Leech, G. na Short, M. (2007). *Style in Fiction. A Linguistic Introduction to Fictional Prose.* New York: Longman Limited.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry.* New York: Routledge

Lugwiri, P. (2011). *Sitiara, Taashira na Tashibihi katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utenzi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimtindo.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili, Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Momanyi, C. (1998) *Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisia katika Utenzi wa Al Inkishafi.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: E.A.E.P.

Mwakio, L. (2016). *Matumizi ya Tashbiha, Sitiari na Taashira katika Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ngunjiri, D. M. ( 2012). *Matumizi ya Taswira kama Kigezo cha Kufanikisha Maudhui Katika Utendi wa Siraji Uliotungwa na Mohamed Kijumwa.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Norgaard, N. etl. (2010). *Key Terms in Stylistics.* New York: Continuum International Publishing Group.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi.* Rock Island: Augustana College.

Nyanchama, M. B. (2004). *Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhiki.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Nyutu, W. J. (2016). *Mtindo katika kazi za kubuni za Leonard Sanja.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Nzilu, M. (2018). *Matumizi ya taswira katika tamthilia za Said A. Mohamed: Pungwa, Kivuli kinaishi na Mashetani wamerudi.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Osiemo, D. (1997). *Fani Katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega, Uhakiki wa Upisho wa Umalenga na Dafina ya Umalenga.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa

Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Evans Brothers.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi*: *Nadharia na Tahakiki.* Dar-es Salaam: Dar-es Salaam University Press.

Shirazi, M. (2005). *The Prophet Muhammad: A Mercy to the World.* Dubai: Create Space Indepedent Publishing platform.

Shitemi, N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne Ishirini.* Eldoret: Moi University Press.

Simpson, P. (2004). *Stylistics*. *A resource book for students.* London: Routledge.

Tambasi, P. *(*2011*). Uhakiki wa Fani Katika Utenzi wa Tambuka: Nadharia ya Umuundo.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2016). *Kichocheo Cha Ushairi.* Nairobi: Vide - Muwa.

Wamitila, K. W. (2008). *Kazi ya Fasihi 1: Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide - Muwa.

Wamitila K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Istillahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.